

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Sita – Tarehe 13 Novemba, 2018

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae. Katibu.

NDG. LINA KITOSI – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa maswali, tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga sasa aulize swali lake.

Na. 71

Wananchi wa Kata ya Iragua kujenga Shule za Msingi

MHE. GOODLUCK A. MLINGA aliuliza:-

Wakazi wa Kata ya Iragua, Vijiji vya Mafinji, Mbenja, Mikochi na Kipingo wamejenga shule za msingi kwa nguvu zao wenyewe na zina muda mrefu sasa.

Je, kwa nini Serikali imeweka vikwazo vya kuzisajili shule hizo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shule za Mafinji, Mbenja, Mikochini na Kipingo zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni vituo vilivyoanzishwa chini ya Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Waliokosa (MEMKWA) ambavyo hutoa elimu kupitia Mpango wa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Vituo hivyo, vilifanyiwa ukaguzi mwaka 2013 na Mdhhibiti Ubora wa Shule akisaidiwa na Mhandisi wa Wilaya na Afisa Ardhi wa Wilaya ili kuona kama vituo hivyo vinaweza kukidhi vigezo vya kusajiliwa kuwa shule za msingi na kuanza kupokea wanafunzi katika mfumo rasmi wa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vitu hivyo havikupata usajili kutokana na upungufu wa miundombinu inayohitajika ili kusajili shule ya msingi. Miundombinu inayohitajika ni pamoja na uwepo wa chumba cha darala la elimu ya awali, vyumba vya darasa la kwanza hadi la saba, vyoo vya walimu, vyoo vya wanafunzi (kwa wavulana uwiano wa tundu moja kwa wanafunzi 25 na wasichana kwa uwiano wa tundu moja kwa wanafunzi 20), eneo lisilopungua ekari saba na nusu kwa vijijini na ekari tatu na nusu kwa maeneo ya mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile baadhi ya maeneo vilipojengwa vituo hivyo yako ndani ya hifadhi chini ya Pori Tengefu la Kilomero. Wizara ya Maliasili na Utalii, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupitia mradi wa *KILORWEMP* zimepanga kupitia upya mpaka wa Pori Tengefu la Kilomero ili kubaini maeneo yatakayokidhi mahitaji ya kisheria kwa ajili ya maendeleo ya wananchi ikiwemo ujenzi wa shule.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Goodluck Mlinga swali la nyongeza.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA:- Asante Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichuke nafasi hii kuipongeza Wizara ya TAMISEMI kwa kupata timu mpya mchezaji mpya, Mwita Waitara Mwikabe. Naomba kuuliza swali langu la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ninavyoongea tayari Wizara zimeshapitia mipaka na kubaini shule ya msingi Mikochi ipo nje ya eneo oevu, na sasa hivi ninavyoongea shule ina madarasa manne, walimu wa tano na vyoo matundu saba na mimi Mbunge naenda kutia nguvu zangu kufikisha madarasa yawe saba. Je, Serikali ipotayari kukagua tena shule hizi na kuzifanyia usajili? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuna mpango wa *EP4R*. Je, Serikali ipo tayari kusaidia shule hili kuboresha miundombinu yake?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHATS. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza naomba kwa niaba ya Wizara ya TAMISEMI nipokee pongezi kutoka kwa Mheshimiwa Mlinga, tunazipokea na tunaahidi tutashirikiana na yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza anasema sasa hivi tayari imeshabainika eneo lile haliko katika eneo oevu na hivyo kwa mujibu wa maelezo yake ni kwamba itakuwa inafaa kuanzisha shule ya msingi. Naomba kwanza ni mhakikishie ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba huduma zinasogezwa jirani na Wananchi na kama ambavyo ameahidi yeye mwenyewe naomba nimpongeze kwamba na yeye ataweka nguvu zake ili kuhakikisha kwamba ile haja ya kuhakikisha kwamba yanakuwepo madarasa kuanzia madarasa mpaka la saba yanakamilika, hakika akikamilisha

kama sisi Serikali tutakuwa tayari kuhakikisha shule inasajiliwa kwa sababu itakuwa imekidhi vigezo ambavyo awali ilisababisha isiweze kusajiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili, anaomba kwamba katika Mpango wa *EP4R* ni vizuri na wao wakawa *considered*, naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwanza takwa la kwanza ni kuhakikisha shule inasajiliwa na shule hili isajiliwe lazima kwanza iwe imekamilisha vyumba vya madarasa saba na ye ameahidi kwamba ataakikisha kwamba ina kamilika, sasa ikishakamilika itakuwa ni raisi sasa hata kuelekeza pesa za *EP4R* kwa sababu tunapeleka sehemu ambayo tayari shule imekwisha kusajiliwa.

NAIBU SPIKA: Niwakumbushe Waheshimiwa mliosimama maswali yanahusu vikwazo vya usajili wa shule, ndiyo maswali ya nyongeza. Mheshimwa Cecilia Paresso.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vikwazo hivyo vya usajili haviko tu katika shule za msingi lakini yapo pia viporo katika vyumba vyetu madarasa katika sekondari zetu nchini, maabara, nyumba za walimu, zahanati zetu kwa maana imetumiaka nguvu za wananchi lakini miradi hiyo haijakamilika, Serikali iko tayari sasa kufanya tathmini kwa upya kuziangalia na kuzikamilisha na zile ambazo zinakidhi usajili ziweze kupatiwa usajili?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza sio vizuri tukaita kwamba ni vikwazo kwa sababu kimsingi kuna *standard* ambazo lazima zifikiwe ili usajili wa shule uweze kufanyika. Naomba nimwambie Mheshimiwa

Pareeso na Wabunge wengine ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba changamoto zinatatuliwa ili huduma ya elimu ziweze kuwafikia watoto wetu kupunguza umbali mrefu wa kufuata elimu na hivi sasa hivi haitazidi mwezi Disemba, tayari Serikali imeshatenga bilioni 54 ambayo tunaenda kufanya ukarabati pamoja na ujenzi ikiwepo vyumba vya madarasa, kumaliza maabara, pamoja na vyoo. Ni azma ya Serikali inaongozwa na CCM kuhakikisha kwamba itatatua kero za wananchi.

NAIBU SPIKA, Mheshimiwa Lubeleje swali kuhusu vikwazo vya usajili.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa walimu wanaishi katika mazingira magumu sana, hawana nyumba tulikuwa na mradi wa MEMM hatukujenga nyumba za walimu tulijenga madarasa, sasa Mheshimiwa Waziri Serikali ina mikakati gani ya kutenga fedha za kutosha ili kuwajengea walimu wa shule za msingi nyumba?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu usajili maana hapa umetaja vigezo kwamba madarasa yawe mangapi na vitu kama hivyo. Lakini shule za msingi kwa sababu zinaanza darasa la kwanza ama na zile za awali, nadhani wananchi wakishajenga madarasa kadhaa wanayoweza kuanza nayo, ni vizuri Serikali iangalie wale wananchi kama wanaweza kuendelea kujenga basi, wapewe kama ni usajili wa muda ili wakati unajitazamia. lakini awezi kujenga madarasa yote saba wakati wanafunzi watakaokuwepo ni wadarasa la kwanza. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge, wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 72

Asilimia ya Mapato kwenda Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR aliuliza:-

Kwa mujibu wa Katiba kuna asilimia ya mapato yanatakiwa yaende Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Je, utekelezaji wa suala hili umefikia wapi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 133 inazungumzia uwepo wa Akaunti ya Fedha ya Pamoja kwa ajili ya miamala ya shughuli za Muungano. Chanzo cha mapato kwa ajili ya shughuli za muungano, yatakayoingizwa kwenye Akaunti ya Pamoja ni mchango kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, Ibara ya 134 ya Katiba inatamka kwamba Tume ya Pamoja ya Fedha itakuwa na jukumu la kupendekeza utaratibu wa kuchangia na kugawana mapato yatokanayo na shughuli za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa uendeshaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha umependekezwa kwenye Ripoti ya Mapendekezo ya Vigezo vya Kugawana Mapato na kuchangia gharama za Muungano iliyoandaliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 2006. Hata hivyo, Akaunti ya Pamoja ya Fedha haijafunguliwa na kuanza kufanya kazi kwa kuwa majadiliano kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mapendekezo ya Tume hayajakamilika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab Bakar swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa akaunti ya pamoja haijafunguliwa hadi leo, ni takribani ni miaka 34. Je, ni lini sasa hiyo akaunti itafunguliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, majadiliano tunaambiwa hayajakamilika ndiyo maana ikawa akaunti hiyo haijafunguliwa, sasa nataka kujua je, Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar inachangia kiasi gani mpaka leo majadiliano hayo hayajakamilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango.

NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza ni lini akaunti itafunguliwa kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba majadiliano yanaendelea kati ya Serikali mbili ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa hiyo, tutakapomaliza majadiliano na kukubaliana kama ilivyoelekezwa na Katiba Ibara ya 34 lazima kuwe na makubaliano Akaunti ya Pamoja itafunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili ni kiasi gani kinachangiwa; kwa mfumo uliopo sasa mapato yate yanayotokana na shughuli za Muungano zinazofanyika Zanzibar huwa yanatakiwa kubaki Zanzibar na kutumika kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na maendeleo katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na mapato yote yanayotokana na shughuli za Muungano ambazo zinafanyika Tanzania Bara basi nayo yote ni makubaliano na mfumo ambao uliopo ndiyo ambayo hutumika Tanzania Bara kwa shughuli zile za Muungano.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Suleiman, swali la nyongeza.

MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu haki ya Zanzibar katika vyanzo vyote vya mapato vya Muungano ni asilimia 4.6 ikiwemo misaada pamoja na mikopo, nataka kujua ni mara ngapi ambapo Zanzibar imepata haki yake kamili ya asilimia 4.6?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba afahamu ni asilimia 4.5 ndiyo ambayo mgao ulivyo na ni mara zote na miaka yote Zanzibar imekuwa mgao huu wa asilimia 4.5 wa yale mapato yanayotakiwa kupelekwa Zanzibar ikiwa ni pamoja ni misaada na mikopo kama alivyosema.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje.

Na. 73

Hitaji la Kituo cha Ushuru wa Forodha na Ukaguzi – Ileje

MHE. JANET Z. MBENE aliuliza:-

Wilaya ya Ileje ipo mpakani mwa nchi za Zambia na Malawi na kuna biashara na mwingiliano mkubwa wa jamii katika eneo hilo. Lakini hayo yote yanafanyika bila utaratibu mzuri wakati mwingine kuhatarisha usalama kwa sababu hapana kituo cha ushuru wa forodha wala soko la kimataifa, hakuna kituo cha uhamiaji, hakuna kituo cha kudhibiti mazao na mifugo na pia hakuna kituo cha ukaguzi wa silaha.

Je, ni lini Serikali itajenga miundombinu hiyo muhimu kwa ufanisi na maendeleo ya Ileje?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto iliyopo ya mwingiliano wa kibiashara baina ya wananchi wa Wilaya ya Ileje, Mkoani Songwe na wananchi wa nchi za Malawi na Zambia. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali imeanza mchakato wa kuanzisha Kituo cha Forodha Isongole mpakani mwa Tanzania na Malawi.

Aidha, mchakato wa kufungua kituo kipya cha forodha unatakiwa kuzingatia Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambayo inaitka nchi mwanachama kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki maombi ya idhini ya kuanzisha kituo kipya cha forodha na hatimaye kutangazwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki (*East Africa Corporation Legal Notice*) ili kupata nguvu ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali imewasilisha maombi ya kufungua Kituo cha Forodha Isongole kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki mwezi Julai, 2018. Pia eneo la kujenga miundombinu ya Ofisi ya Forodha Isongole limepatikana na taratibu za kupata hatimiliki zinaendelea. Aidha, ujenzi wa miundombinu utaaanza mara idhini ya kuanzisha kituo hicho itakapotolewa na kutangazwa kwenye Gazeti la Jumuiya ya Afrika Mashariki na hatimiliki ya eneo husika kupatikana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Janet Mbene swali la nyongeza.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwanza kabla sijauliza swali la nyongeza niipongeze sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa sikivu, tumeomba hiki kituo muda mrefu lakini hatimaye tunaona kinaenda kufanyiwa kazi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri nashukuru sana Serikali. (*Makofi*)

Naomba sasa niulizwe swali moja tu la nyongeza kuwa Isongole ni kata ambayo ni ya kibishara sana kutokana na *position* yake katika mpaka huu na tumekuwa tukiomba Serikali itujengee soko la kimataifa pale kwa sababu hizohizo za kibiashara pamoja, siyo na Malawi na Zambia tu hata na DRC.

Je, Serikali ipo tayari sasa kutokana na maendeleo ya barabara inayojengwa pale na hiki Kituo cha Forodha kinachokuja kujitokeza kutuwekea soko la kimataifa? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ipo tayari kufanya shughuli za maendeleo popote pale ambapo wananchi wetu wanashughulika na shughuli za kiuchumi, naomba nimuahidi Mheshimiwa Janet kwamba sisi kama Serikali na hasa Wizara ya Fedha na Mipango tutakwenda kufanya tathimini na tutakapojiridhisha kwamba sasa tuko tayari kufanya hayo maendeleo hayo anayoyasema ya Kituo cha Kimataifa tupo tayari kama Serikali kwenda kujenga lakini tuingiza kwenye mipango yetu ya Serikali kama taratibu zinavyotuelekeza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K.MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kuongeza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Serikali imefanya nzuri sana kwenye mpaka wa Wilaya Momba mpaka wa Zambia na Tanzania kwa kulasimisha matumizi ya sarafu ya Zambia na ya Tanzania ili kukomesha magendo na ulanguzi, Serikali inasemaje kuhusu mpaka kati ya Malawi na Tanzania na Kituo cha Isongole na kufanya kazi kama hiyo hiyo? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea pongezi za kurasimisha sarafu pale mpakani na huku mpaka anaoutaja upande huu alioutaja kama Serikali tunaenda kulifanyia kazi na naamini kama tuliweza kurasimisha upande mmoja tutaweza pia na upande uliobaki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deo Ngalawa swali la nyongeza.

MHE. DEO F. NGALAWA: Mheshimwa Naibu Spika, ahsante sana, kama ilivyo Wilaya ya Ileje kuwa imepakana na nchi za Malawi na Zambia pia Wilaya ya Ludewa imepakana na nchi ya Malawi; na ikumbukwe Wilaya ya Ludewa ni mzalishaji mkubwa sana wa mahindi pengine kuliko hata maeneo maengine yoyote.

Je, ni lini sasa Serikali itaona kuna haja ya kuweka vituo vya forodha katika vijiji vya Manda na Lupingu ili kurasimisha na biashara zingine ziweze kwenda katika namna ambayo inafaa?

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Deo Ngalawa amekuwa akilifuatilia jambo hili sana na nimeshaka naye mara kujadiliana kuhusu kujenga kituo hiki cha forodha katika vijiji vya Manda na Lupingu, na tayari tangu tulilivyo fanya

majadiliano Mheshimwa Ngalawa nilishawapa maelekezo mamlaka ya mapato Tanzania waende wakafanye tathimini na sasa wako tayari kuingiza kwenye mipango yao kuhakikisha kituo hiki cha forodha kina jengwa kulinga na sheria za zinavyotuelekeza.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Neema William Mgaya Mbunge wa viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 74

Azimio Kuhusu Masuala ya Demokrasia, Chaguzi na Utawala Bora

MHE. NEEMA W. MGAYA aliuliza:-

Miaka sita iliyopita Serikali ya Tanzania ilishiriki na kupitisha Azimio kuhusu Masuala ya Demokrasia, Chaguzi na Utawala Bora lililopitishwa na Umoja wa Afrika.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni kwa nini hadi sasa Azimio hilo halijaridhiwa na kusainiwa rasmi?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha Azimio hilo linaridhiwa na kusainiwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuiteua kuwa Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Nje Ushirikiano wa Kimataifa ili niweze kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Balozi Augustine Philip Maiga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa naiba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki - Dkt. Balozi Augustine Philip Maiga ambaye yupo ndani hapa Bungeni leo hii, napenda kujibu swali la Mheshimwa Neema William Mgaya, Mbunge wa Viti Maalum lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Afrika kuhusu Demokrasia. Chaguzi na Utawala Bora yaani *African Charter on Democracy, Elections and Governance* ulipotishwa na Umoja wa Afrika wakati wa Mkutano wa Wakuu wananchi na Serikali wa Umoja wa Afrika tarehe 30 Januari, 2007. Lengo la mkataba huu ni kuzitaka nchi wanachama kuzingatia na kutekeleza utawala bora, utawala wa sheria na haki za bindamu kama ilivyoelezwa katika ibara ya 3 na 4 ya mkataba huo. Hadi hivi sasa ni jumla ya nchi wanachama 35 tu ndizo zimeridhia mkataba huo ilihali nchi 19 bado hazijaridha ikiwemo Tanzania.

Mheshimwa Naibu Spika, naomba kulieleza Bunge lako tukufu kuwa sababu zinazoifanya Tanzania isitie au ichelewe kuweka saini na kuridhia mkataba huo ni kutokana na kuwepo ibara ambazo zipo kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria zetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Neema Mgaya swali la nyongeza.

MHE. NEEMA W. MGAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikari itafanya mabadiliko ya mkataba ili uweze kuendana na Katiba ya nchi yetu? Swali la kwanza hilo.

Swali la pili nilitaka kujua kwa kutosaini mkataba huu vipi kuhusu usimamizi wa masuala ya uchaguzi, demokrasi yanakwendaje? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki majibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimwa Naibu Spika, ahsante sana awali ya yote Neema Mgaya kwa swali lake zuri na lenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa, nchi inaangalia vigezo vingi mbalimbali ikiwepo ukinzani wa mikataba hiyo na sheria zetu za ndani, Katiba pamoja na tamaduni nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kama zilivyokuwa nchi zingine 19 tunafanya mchakato wa ndani wa kuangalia ni kwa jinsi gani tunaweza tukarekebisha ama sheria zetu za ndani ama kurudi kwenye *AU* na kuomba vifungu kadhaa kwenye mkataba huo virekebishwa ili viendane na sheria na Katiba yetu na hilo likikamilika kama ambavyo tumeridha mikataba mingine mbalimbali na mkataba huu pia utaridhiwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Mtolea swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu ya Serikali yanasema vipo baadhi ya vipengele haviendi sawa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio maana Serikali inachele kuridhia mkataba huu, na mkataba huu unahusu demokrasia, changuzi...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa, uliza swali.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: ...kwa majibu haya sasa Serikali inakiri kwamba namna ambavyo tunaendesha demokrasia, chaguzi na utawala bora hapa nchini ni kinyume na mataifa mengine ya Afrika? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimwa Naibu Spika, ahsante, masuala ya uchaguzi, demokrasia na utawala bora yanaratibiwa vilivyo na ipasavyo kwa kuzingatia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kwa kuzingatia Sheria ya Uchaguzi pamoja na kanuni zake mbalimbali, pia kwa kuangalia sheria mbalimbali ambazo zinaratibu suala nzima la utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni mhakikishie Mheshimwa Mbunge kwamba masuala hayo yanaendeshwa vizuri na ndio maana tuna Katiba, tuna Sheria ya Uchaguzi ambayo imemuweka leo yeye Bungeni hapa ndani. Nimhakikishie kwamba Tanzania itaendelea kuheshimu suala la utawala bora, suala la demokrasia na lakini pia itaendesha uchaguzi wake kwa uhuru kwa haki na amani. *(Makoff)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli ulio wazi kwamba Tanzania tumekuwa tukiridhia maazimio mabalimbali na mengi sana, lakini *domestication* imekuta tatizo kubwa sana. Nilitaka kujua nafasi ya Wizara hii katika kuhakikisha kwamba maazimio yote ambayo tumeyaazimia yanakuwa *domesticated*, mfano *CEDAW*, *Africa Union* kwa lile suala la asilimia 50 kwa 50 kuwa katika maamuzi ni kwa jinsi gani Wizara yenu inatekeleza hayo maazimio ambayo tumeridhia?

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki majibu

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba Tanzania inatekeleza vizuri sana mikataba ya mbalimbali ya kimataifa ambayo tumeshairidhi, lakini sio mikataba yote tunaweza kukairidhia kwa sababu mikataba mingine ina kinzana na misingi ambayo tumejiwekea, misingi ya kikatiba, mila, desturi na utamaduni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumekuwepo na mijadala mingi sana hapa kuhusu masuala ya ushoga na masuala mengine, hiyo masuala ushoga yanatokana na mikataba ya kimataifa sio kila mkataba tunaweza tukauridhia, lakini kuhusu swali lake la haki sawa kwa jinsia zote hasa 50 kwa 50. Tanzania moja kati ya nchi ambayo imetekeleza sualahilo kuhakikisha kwamba tuna Viti Maalum kuongeza uwakilishi wa wanawake katika Bunge hili na katika nafasi nyingine za uongozi Serikalini. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwamoto swali la nyongeza.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi wa tano Marais wa Afrika walikutana na walikubaliana waweze kuridhia *protocol* ya Malabo ili kufanya Bunge la Afrika kuwa huru.

Je, nini msimamo wa nchi yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimwa Naibu Spika, ahsante sana, Bunge la Afrika limeanzishwa kwa mujibu wa taratibu na Kanuni za *AU* na kwa mujibu wa taratibu hilo Bunge ni huru kama chombo cha *AU* inatekeleza majukumu yake kwa

uhuru kabisa na hata sisi katika Bunge hili tuna wawakilishi katika Bunge la Afrika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Malabo unaongelea mambo mengi sio tu kuhusiana Bunge la Afrika. Mambo ambayo yanahusu masuala mengi ya haki za bindamu na uwekezaji na Utawala Bora kwa Afrika kwa hiyo nimuhakikishie Mheshimiwa Mwamoto kwamba Bunge la Afrika lipo huru na litendelea kuwa huru. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Saada Mkuya swali la nyongeza.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amezungumza kuna baadhi ya vipengele vya hii *chartery* demokrasia, uchaguzi na utawala bora vinakinzana sana na Katiba yetu pamoja na sheria zingine, labda *specifically* ni vifungu gani katika hiyo *charter* vinakinzana ili tuone kwa utaratibu gani tunaweza tukavirekebisha ama tukaomba AU wakarekebisha kulinga na mazingira yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimwa Naibu Waziri hilo swali litahitaji majibu ya baadae kwa sababu hivyo vifungu hautakuwa na mkataba hapo sasa hivi.

Waheshimwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Martha Moses Mlata sasa aulize swali lake.

Na. 75

Wimbo Maalum wa Afrika Mashariki

MHE. MARTHA M. MLATA aliuza:-

Je, Tanzania ilishiriki kwa namna gani katika mchakato wa kuupata Wimbo Maalum wa Afrika Mashariki?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Balozi Augustine Philip Maiga, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum naomba kutoa ufafanuzi kuwa huu si wimbo maalum ni wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kama zilivyo nyimbo nyingine za Taifa katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya ufafanuzi huo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Moses Mlata, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wa kuupata wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulifanywa na nchi tatu waanzilishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yaani Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Uganda ambapo lilitolewa tangazo la kuwapata watunzi kutoka katika nchi hizi tatu ambazo kwa wakati huo ndiyo zilikuwa nchi wanachama. Baada ya tangazo kutolewa kila nchi iliwasilisha wimbo mmoja katika Mkutano wa Nane wa Wakuu wa Nchi uliofanyika mjini Arusha tarehe 30 Novemba, 2006. Kwa hiyo, katika hatua hii tulikuwa na nyimbo tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyimbo zote tatu ziliimbwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi uliofanyika Kampala, Uganda mwezi Novemba, 2017. Wakuu wa Nchi wakaagiza nchi za Rwanda na Burundi ambazo ndiyo kwanza zilikuwa zimejiunga na Jumuiya kutoa maoni yao katika nyimbo hizo tatu zilizoimbwa.

Aidha, Wakuu wa Nchi hao waliagiza ziandaliwe nyimbo mbili kutokana na nyimbo tatu zilizoimbwa. Uamuzi huu ulifikiwa ili kuondoa changamoto ya kuwa na wimbo wa jumuiya ulioandaliwa na nchi moja.

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi uliofanyika Kigali, Rwanda mwezi Aprili, 2009 nyimbo mbili ziliimbwa ukiwemo wimbo wenye maneno mengi ya mtaalam wa Kiswahili kutoka Tanzania, Profesa Hermas Mwansoko, ambaye wakati huo alikuwa Mkurugenzi wa Utamaduni, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

Mheshimiwa Spika, Mchakato huu haukuishia hapo kwani katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi uliofanyika Ngurdoto, Arusha mwezi Disemba, 2010 aliamuliwa kwamba ziunganishwe sintaksi za nyimbo hizo mbili ili kupata wimbo mmoja. Sintaksi yaani msuko wa sentensi za lugha ya kiswahili katika wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ziliandaliwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilishiriki kikamilifu katika mchakato wote wa kuandaa wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Martha Mlata, swali la nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwanza nimpondeze Mheshimiwa Naibu wa waziri kwa majibu Mazuri ambayo ameyatoa na kweli alichoeleza hapa ni sahihi na huo wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki alivyosema sio maalum ni wimbo na mimi nasema ni wimbo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa maswali yangu mawili, kwanza kabisa mchakato aliuleza katika kuwapata watunzi ni kweli walitoka nchi hizo tano kama alivyosema na walivyofika kule kulikuwa na makubaliano rasmi au maalum vyovyote, lakini kwa makubaliano yale ninaomba aniambie ni staiki gani mtunzi kutoka Tanzania ambaye anaitwa John Joseph Mgango kutoka Bukoba alizipata kutokana na makubaliano yale?

Je, yale makubaliano yote yaliyofanywa na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa watunzi wa nchi zote tano ili kuweka

kumbukumbu sahihi kwamba kila nchi imeshiriki katika kutunga wimbo huo, ni yapi ambayo yametokelezwa, yapi ambayo yanatekelezwa, ni lini yatatekelezwa yote na kuwapa stahiki zote watunzi wa nyimbo hizi? Ahsante. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri nitakupa uhuru kama hayo maswali utayajibu baadae kwa sababu yanahitaji taarifa rasmi lakini kama unayo unaweza kujibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato huu uliendeshwa Jumuiya ya Afrika na Sekretarieti ya Afrika Mashariki ndio ilikuwa inaendesha mchakato mzima. Tarehe 12 Oktoba, 2018 Wizara ilipokea barua kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Mchezo kwamba kuna Mtanzania huyo kwamba anadai stahiki zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tumewasiliana tayari na Jumuiya ya Afrika Mashariki na tunasubiri majibu kuona makubaliano hayo kati ya mtunzi huyu na Jumuiya yalikuwaje na yalitekelezwa kiasi gani na nini tufanye ili kumsaidia kuona kama haki yake bado ipo. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Moshi Kakoso, swali la nyongeza.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, Shirika la *Kenya Airways* ni Shirika la Ndege ambalo linatumia nembo ya jina Mlima Kilimanjaro kwenye baadhi ya ndege zake na kufanya mataifa ya nje yaamini kwamba Mlima Kilimanjaro unatoka nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Serikali imechukua hatua gani kudhibiti kitendo kama hiki ambacho kinaipotezea mapato ya nchi yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salma Kikwete swali la nyongeza.

MHE. SALMA R. KIKWETE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kutokana na swali la msingi, na mimi naomba niulize swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zote duniani zina wimbo wake wa Taifa, na wimbo wa Taifa una taratibu rasmi wakati unaimbwa, sisi kama Tanzania, tuna wimbo wetu vilevile wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni upi wakati wa kuimba Wimbo wa Taifa kwa sababu wengine ukiimbwa Wimbo wa Taifa wanasimama kikakamavu, wengine ukiimbwa wimbo wa Taifa wanashika hapa (kifua) sasa kati ya hayo ni lipi kwa wimbo wetu wa Taifa wa Tanzania? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za wakati wa kuimba wimbo wa Taifa ni kwamba tunafuata ukakamavu wa kijeshi, tunaweka mikono yote miwili chini, unasimama kama vile uko katika gwaride la Jeshi ukiwa mkakamavu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 76

Zao la Alizeti Kukosa Soko

MHE. JUSTIN J. MONKO aliuliza:-

Wenye viwanda, vya kukamulia alizeti wamekuwa wakilalamika kukosa alizeti na wakati huo huo wakulima wamekuwa wakibaki na alizeti kwa kukosa wanunuzi.

(a) Je, ni nini kauli ya Serikali juu ya hali hiyo ya wakulima kukosa soko la alizeti?

(b) Je, Serikali ipo tayari kununua alizeti kwa wakulima ili wapate fedha za kuendesha maisha yao na kujiandaa kwa msimu mwingine wa kilimo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa niaba ya Waziri, wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin Joseph Monko, Mbunge wa Singida Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia maonesho mbali mbali ikiwemo maonesho ya Sabasaba na SIDO na kwa kupitia Kongano za Alizeti imekuwa ikiwakutanisha wakulima wa alizeti, watafiti na wazalishaji wa mafuta wa ndani na nje ya nchi ili kukidhi mahitaji ya soko la alizeti na mafuta kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha wakulima wanapata soko, Serikali imeendelea na juhudi za kuweka mazingira bora ya uwekezaji ili kuvutia ujenzi wa viwanda vya kusindika mbegu za mafuta ikiwemo zao la alizeti. Mpaka sasa kuna zaidi ya viwanda 20 vya kusindika mbegu za mafuta vyenye *crushing capacity* tani 1,445,000 na *refining capacity* tani 295,000. Aidha, Chama cha Wasindikaji wa Alizeti Tanzania (*Tanzania Sunflower Processors Association – TASUPA*) kimeendelea kushirikiana na wakulima kwa kwa kununua na kusindika alizeti inayozalishwa hapa nchini, ikiwa ni pamoja na kulipia gharama za usindikaji wa mafuta yanayopatikana na kutafuta soko lenye tija. Vilevile katika kulinda na kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya mafuta ya kula yanayozalishwa nchini Serikali imeweka kiwango cha

asilimia 35 kwa uingizwaji wa mafuta safi na asilimia 25 kwa mafuta ghafi kutoka nje ya nchi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Justin Monko swali la nyongeza.

MHE. JUSTIN J. MONKO: Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Awali ya yote ningependa uniwie radhi niseme kwamba naona majibu yangu maswali niliyouliza ni kama yamepata majibu ya kisanii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu spika, nilitaka kujua kauli ya Serikali kuhusiana na sakata hili kwamba wakulima wa Singida Kaskazini wamebaki na alizeti majumbani wakati viwanda vyetu havina malighafi za kutosha kwa sababu wameendelea kuwatumia madalali kuchukua kwa bei ndogo. Sasa kauli ya Serikali hapa naambiwa habari ya *SIDO* Maonesho ya *SIDO*, Maonesho ya Sabasaba, kiukweli hili linasikitisha sana.

Sasa kama hii ndio kauli ya Serikali nilitaka niulize je, Mheshimiwa Naibu Waziri sasa yuko tayari kuwasafirisha wakulima wa Mkoa wa Singida ili waende wote kwenye Maonesho ya Sabasaba na Nanenane ili waende sasa wakajifunze na kukutanishwa na hao wasindikaji?

Swali la pili, nilitaka kujua kama Serikali iko tayari sasa kununua alizeti hiyo ili Wananchi waweze kupata fedha? Lakini sasa hapa nimepewa...

NAIBU SPIKA: Umeshauliza mawili Mheshimiwa, maswali mawili. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, akutukanaye hakuchagulii tusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama yeye kwenye swali alijua kwamba tatizo ni madalali pengine swali lingesema moja kwa moja ni madalali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu kuwasafirisha wananchi wote kuwapeleka kwenye *SIDO*, sio utaratibu unaotumika, lakini matangazo yamekuwa yakitolewa na yeye mwenyewe ni shahidi pia hata kupitia katika *cluster* ambayo ipo Ntinku tumeendelea kuwakutanisha pamoja na watafiti mbalimbali kwa hiyo mimi nilitegemea kwamba jibu ambalo tumemjibu atahusisha na hata *cluster* ambayo ni Kongani ipo katika eneo lake la Ntiku.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sware Semesi, swali la nyongeza.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na sintofahamu kwa soko ya mazao ya biashara si tu kwa alizeti hususani pia kwenye mazao ya mbaazi na mtama mweupe. Sasa ni nini mkakati wa Serikali kuweza kutoa huduma kwa wananchi hao wanaoteseka na mazao yao na kuwaongezea umaskini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIAHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutafuta masoko na hata jana tu kupitia hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli amezidi kutuagiza kwamba tufanye kasi katika kuhakikisha kwamba mazao mengi yanapata soko kupitia taasisi zetu ikiwemo *TANTRADE*. Kwa hiyo. tutaendelea kufanya hivyo, lakini vilevile kuendelea kuhamasisha wananchi kutumia fursa ya mazao yanayopatikana nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kwa kunipa fursa na mimi kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mikoa ya Dodoma na Singida ni miongoni mwa mikoa katika nchi hii ambayo inazalisha zao la alizeti kwa wingi sana.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga soko maalum la alizeti katika Mkoa wa Singida ili wenye viwanda, na wawekezaji wawe na eneo maalum la kununua alizeti ili wenye viwanda na wakulima waweze kupata tija? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali imeona umuhimu wa kufanya hivyo na tayari imeshatenga eneo kwa ajili ya kuwezesha wakulima waweze kupata eneo la kupata soko pamoja na kuongeza thamani ambalo lipo katika eneo la Zuzu, kwa hiyo, naamini fedha zikipatikana soko hilo litaweza kuendelezwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mariam Ditopile swali la nyongeza.

MHE. MARIAM D. MZUZURI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuwa Wakulima wa Mkoa wa Dodoma pia wamekuwa wanalima alizeti kwa wingi, na pia tumeona juhudi za Serikali katika kuwekeza kwenye viwanda vya kukamua mafuta haya lakini, kumekuwa na malalamiko makubwa sana ya mizani ambayo inapimia alizeti hizi kule kiwandani na inawezekana hiyo ndiyo sababu kubwa wakulima hawa, wanavunjika moyo kwenda kuuza alizeti zao viwandani huko.

Je, Serikali imejipanga vipi na inatumia aina gani ya vipimo kuhakikisha hizi mizani hazichezewi na zinatoa kilo halisi? Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIAHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ziko changamoto mbalimbali kuhusiana na zao hili la alizeti, mojawapo ikiwa ni hivyo vipimo, kama alivyosema, lakini vilevile ni pamoja na uhafifu wa mbegu zinazotumika katika uzalishaji wa mafuta haya ya alizeti, Serikali imeliona hilo, kupitia taasisi yetu ya Vipimo, tunaendelea kukagua mizani na kuhakikisha kwamba mizani inafuata taratibu na Viwango vilivyoweka lakini vilevile, kuhamasisha wakulima kutumia mbegu bora ili alizeti hizo ziweze kuwa na uzito unaokidhi na kuweza kutoa mafuta yanayostahili.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Seleman Said Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Ally Saleh.

Na. 77

Hitaji la Elimu ya Uvuvi wa Kisasa - Ukanda wa Pwani

MHE. ALLY SALEH ALLY (K.n.y. MHE. SELEMAN S. BUNGARA) aliuliza:-

Wavuvi wengi wanakabiliwa na tatizo la kutokuwa na elimu ya uvuvi wa kisasa ambapo wengi wao hutumia zana duni za uvuvi hali ambayo haiwaletei tija wavuvi hao na uvuvi ni sekta mojawapo inayochukua vijana wengi hususan kwenye Ukanda wa Pwani.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia wavuvi hao elimu ya uvuvi bora ili uvuvi wao uwe wenye tija?

(b) Je, Waziri atakuwa tayari kuwatembelea na kukutana na wavuvi kwa nia ya kujua changamoto zinazowakabili na kuzipatia ufumbuzi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seleman Said Bungara, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa mpango mkakati wa kuboresha sekta ya uvuvi ambao unalenga kuboresha uvuvi nchini ikiwemo kutoa elimu ya uvuvi wa kisasa kwa wavuvi; kusambaza teknolojia za uvuvi na kuboresha zana za uvuvi. Pia mpango unazingatia wavuvi kupatiwa elimu ya uvuvi endelevu ili kuhakikisha uvuvi nchini unaleta tija kwa wavuvi na Taifa kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Mifugo na Uvuvi amekuwa na utaratibu wa kutembelea wavuvi na wafugaji ili kujua matatizo na changamoto zinazowakabili. Aidha, kwa mwaka huu 2018 Naibu Waziri alitembelea katika Wilaya ya Kilwa katika Vijiji vya Kilwa Kivinje na Somanga na kusikia changamoto zinazowakabili wavuvi pamoja na wafugaji ambapo alitoa maagizo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kushughulikia matatizo yao na matatizo mengine yanaendelea kutatuliwa na Wizara. Kwa mfano tatizo la kuharibika kwa dagaa wakati wa mvua za masika ambapo Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti ya *TAFIRI* na kwa kushirikiana na *VETA* inawatafutia majiko banifu yanayotumia teknolojia rahisi itakayowasaidia wavuvi kuondokana na upotevu wa dagaa yaani *post harvest loss* katika kipindi hicho.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ally Saleh swali la nyongeza.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza, kwa kweli sekta ya uvuvi inaweza kuitoa Tanzania kiuchumi kwa sababu bado hatujatumia fursa ya ukanda wa bahari wa mile 1400 na pia eneo la *economic zone*.

Sasa je, ni lini sasa Mkakati huo wanaosema Waziri utawafikia kwa vitendo ili kuwatoa wavuvi wa Kilwa na Watanzania katika umaskini ambao si wa lazima?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, moja ya njia bora kabisa ya kuwa na uvuvi wa kisasa ni kuwa na sera ya uvuvi wa bahari wa kuu na wa mwambao yaani *blue economy*.

Je, Serikali sasa, itakuwa imejitayarisha kiasi gani kutengeneza Sera hiyo ili *io-compas* suala zima la Uvuvi ili Tanzania iweze kufaidika na Uvuvi ambao hadi hivi sasa hatujautumia kiasi cha kutosha.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini tutaanza kutekeleza mkakati huu, hivi sasa tumeshaanza kutekeleza mkakati huu, wa kuhakikisha sekta ya uvuvi inaleta tija katika Taifa letu na kwa kuanzia tumefufua Shirika letu la Taifa la Uvuvi yaani *TAFICO* tayari tuna *management* na katika kuhakikisha kwamba tunakwenda mbele na kuitumia vizuri rasilimali hii *TAFICO* inakwenda kushirikiana na hata sekta binafsi kununua meli za uvuvi ili tuhakikishe kuwa tunapata manufaa na bahari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ameuliza tumejitayarishaje ili kunufaika na bahari yetu. Tumejitayarisha vyema sana na ndio maana hivi sana tunakwenda katika ujenzi wa bandari ya uvuvi ambapo mshauri mwelekezi yuko kazini toka mwezi wa saba mwaka huu na ifikapo mwezi Februari 2019 atakuwa amekamilisha kazi ya kutuelekeza wapi tujenge bandari ya uvuvi na namna gani tujenge bandari ya uvuvi ambapo hii itatusaidia katika kufanya mavuvi yetu ya kisasa na kupata tija kwa ajili ya maendelea ya Taifa yetu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani swali la nyongeza.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, kuna *operation* ambayo inaendelea hivi sana katika ziwa Tanganyika, ambayo imegubikwa na unyanyasaji mkubwa kwa Wavuvi pamoja na rushwa.

Je, Serikali iko tayari, kusitisha kwanza zoezi hilo badala yake ikajikita kutoa elimu ili kutoa matokeo chanya?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wakati ukija hapa mbele, Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena kabla hujasimama soma swali la msingi linauliza kuhusu nini. Niwakumbushe tena, soma swali la msingi linahusu kitu gani kabla hujaomba swali la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Wizara yetu inaendesha oparesheni, na tunaita *Operation Sangara*. *Operation* hii inafanyika kwa mujibu wa sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009 tuhuma hizi anazozitoa Mheshimiwa Aida, naomba kama ana *specific issue* inayohusiana na haya anayoyasema ya unyanyaswaji wa Wavuvi na Rushwa atuletee Wizarani kwetu nasi tutashughulikia mara moja.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vedastus Manyinyi swali la nyongeza.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipatia nafasi niweze kuuliza swali swali dogo la nyongeza.

Pamoja na mikakati mizuri ambayo watu wa Idara ya Uvuvi wanayo ya kuzuia Uvuvi haramu lakini kumekuwa na changamoto kubwa mfano, katika zile adhabu wanazozitoa katika kukomesha tatizo hili, leo akishikwa muendesha bodaboda akiwa amepakia samaki ambao ni haramu, anapigwa faini kati shilingi milioni mbili mpaka shilingi milioni tatu, ambapo bei ya kununua bodaboda ni kati ya shilingi milioni moja na nusu mpaka milioni mbili, na kutokana na hali

hiyo yule muendesha bodaboda analazimika ku-*surrender* ile...

NAIBU SPIKA: Uliza swali Mheshimiwa.

MHE. VEDASTUS M. MANYINYI: Serikali haioni kama kuna haja ya kuwapa viwango wanavyoweza kuvilipa kulliko kuendelea kupoteza ile bodaboda?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, tozo na faini zote zinazotolewa na Wizara yetu wakati oparesheni zipo kwa mujibu wa sheria yetu, lakini naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Manyinyi na Waheshimiwa Wabunge wengine wote ya kwamba hatumkamati mtu na kumtoa kwa sababu amesafirisha samaki katika bodaboda. Naomba niwaeleze ya kwamba tumetoa mwongozo wa namna ambavyo mtu anatakiwa apigwe faini, kwa hivyo naomba niwatoe hofu na kama liko tatizo la namna hiyo mtu amekamatwa kisa amebeba katika bodaboda, bodaboda ni chombo kinachoruhusiwa kubeba samaki, isipokuwa abebe katika *cooler*, lile lenye kuhifadhi samaki wabichi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tunajua mazingira ya vijijini na sisi tunataka Watanzania wanufaika na rasilimali zao.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hasna Mwilima swali la nyongeza.

MHE. HASNA S. K. MWILIMA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na majibu ya swali la nyongeza sasa hivi aliyoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri kamba wao kama Wizara wametoa mwongozo wa namna gani faini zipigwe kwa vyombo vinavyobeba samaki. Mimi ninao ushahidi na nilimpigia simu Naibu Waziri, gari la abiria limebeba mama aliyekuwa anakwenda kwenye msiba na samaki 20, mwenye gari katozwa faini shilingi milioni 15.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni kweli sheria yao ndiyo inavyowalinda kwamba mwenye gari atozwe faini ya shilingi milioni 15 kwa ajili ya kubeba abiria aliyebeba samaki watano, 10 au samaki 20. Je, kwa nini sasa Wizara isitoe tamko ni kiasi gani wanatakiwa kutozwa kama faini ili nchi nzima tufahamu? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri kama unazo hizo takwimu za ni kiasi gani unaweza kujibu, kama huna takwimu ya ni kiasi gani unaweza ukalijibu baadae, nakupa uhuru huo.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Hasna Mwilima na umenipa *option* ya kwamba je, ni kiasi gani kinachotakiwa. Mheshimiwa Hasna Mwilima na Waheshimiwa Wabunge wote narudia kusema kwamba faini zetu zipo kwa mujibu wa sheria yetu wenyewe ya Bunge la Jamhuri ya Muungano la Tanzania, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ipo wazi inaeleza viwango vya faini ambazo zinapaswa kupigwa katika makosa mbalimbali yanayofanywa katika tasnia hiyo ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa jambo ambalo ni mahususi alilolisema Mheshimiwa Hasna Mwilima kama anahisi lipo tatizo tunnamkaribisha na milango yetu iko wazi, tuweze kujadiliana na kama kweli kipo kosa lililofanyika katika eneo hilo tutarekebisha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma sasa aulize swali lake.

Na. 78

Huduma kwa Wagonjwa Wenye Magojwa Sugu

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawahudumia watu wenye magonjwa sugu kwa asilimia mia moja mfano wagonjwa wa moyo na magonjwa mengine ili kuondokana na adha ya kuombaomba michango na kusababisha vifo kwa wagonjwa wanaokosa michango hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Frank George Mwakajoka, Mbunge wa Tunduma kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la magonjwa sugu ikiwa ni pamoja na magonjwa ya moyo, mishipa ya fahamu, saratani, kisukari, magonjwa sugu ya figo na magonjwa na mengineyo ambayo kitaalamu hujulikana kama magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Utafiti wa viashiria vya magonjwa haya uliofanywa na *STEP* hapa nchini mwaka 2012 na ulio Shirikisha Wizara ya Afya, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu na Shirika la Afya Duniani ulionyesha kuongezeka kwa ugonjwa wa kisukari hadi kufikia 9% ukilinganisha na utafiti uliofanywa mwaka 1980 ambapo kulikuwa na Watanzania chini ya asilimia moja tu wenye kisukari.

Aidha, utafiti huo ulionyesha kuwa asilimia 25.9 ya Watanzania wana shinikizo la juu la damu ukilinganisha na ule wa mwaka 1980 ambapo ilikuwa ni asilimia 2.7 tu wenye shinikizo la juu la damu. Kwa kutambua ongezeko la magonjwa yasiyo ya kuambukiza, Wizara yangu ilianzisha sehemu ya kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza na kutengeneza mkakati wa kupambana na magonjwa hayo wa mwaka 2009 – 2015 na hivi sasa tuna mkakati wa pili wa 2016-2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2007 inatoa mwongozo kwa wananchi kuchangia huduma za afya. Aidha, imeainisha makundi yanayostahili kupata msamaha wa kulipia huduma za afya katika vituo vyote vya kutolea huduma vya umma. Makundi yanayopewa kipaumbele ni pamoja na watoto wa umri wa chini ya miaka mitano, wanawake wajawazito na wazee wenye miaka 60 na kuendelea wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikigharamia baadhi ya huduma za matibabu kwa watu wenye magonjwa sugu katika hospitali za ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, hali halisi imeonyesha kuwa siyo rahisi kuwahudumia wagonjwa hawa kwa asilimia mia moja kwani gharama zake ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kwa wananchi ni kujitahidi kwa nguvu zote kujikinga na magonjwa haya kwa kufanya mazoezi mara kwa mara, kutokutumia tumbaku na kuacha matumizi ya pombe kupita kiasi na kula mlo wenye afya hususan mbogamboga, matunda, kuepuka kula vyakula vingi vya nafaka iliyokobolewa, sukari nyingi pia mafuta yatokanayo na wanyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninatoa rai kwa wananchi kujiunga na mifuko ya bima ya afya ili kuwa na uhakika wa matibabu kabla ya kuugua. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Frank George Mwakajoka swali la nyongeza.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Waziri lakini swali langu halijajibiwa. Mimi nilichokuwa nauliza ni kuhusiana na huduma ya matibabu kwa wagonjwa mahususi wa magonjwa sugu bila kujali jinsia wala umri, lakini kilichotokea Mheshimiwa Waziri ameeleza zaidi utafiti na mambo mengine ambayo yamekuwa yakitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukweli tu ni kwamba ninayo mifano michache ambayo ningeomba niitoe, mfono kuna mtoto mmoja anaitwa Hyasinta Zaya anatokea Matai, Mkoa wa Rukwa ameanza matibabu akiwa na miaka tisa mwaka 2013 na mpaka leo hajapata matibabu na alitakiwa kufanyiwa upasuaji kipindi chote hicho. Wazazi wake walikosa fedha shilingi milioni 10 za matibabu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inawatibu wananchi bure ambao wanakosa fedha za matibabu ili kuokoa maisha ya watazania walio wengi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wazee wengi katika Taifa hili wametumia nguvu zao nyingi sana kulijenga Taifa hili, lakini wazee hawa sasa hivi hawana uwezo wa kuhimili gharama za matibabu hasa matibabu sugu kama figo pamoja na magonjwa mengine ya moyo. Serikali ina mpango gani wa kuwapa bima ya afya ili wazee hawa waweze kutibiwa bure kuliko usumbufu unaojitokeza sasa hivi ambapo wazee hawa wanakosa matibabu? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mwakajoka kwa maswali yake mazuri mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza umeuliza kwa nini Serikali isigharamie kwa asilimia 100 matibabu ya magonjwa sugu. Sasa siwezi kusema tu lazima utoe angalau ka-*preamble* kuonesha hali halisi ya ongezeko la magonjwa haya na njia kubwa ya kupambana na magonjwa sugu ni kinga. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kuwaonesha hali halisi Watanzania, wapi tumetoka na wapi tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mtoto Hyasinta ambaye umetoa taarifa hapa kwamba ana tatizo la ugonjwa wa moyo na amekosa matibabu, zipo taratibu za

kufuata. Juzi *Jakaya Kikwete Cardiac Institute* imetoa matibabu bure kwa watoto zaidi ya 50 wamefanyiwa upasuaji kwa kushirikiana na madaktari kutoka Israel. Kwa hiyo, utaratibu upo na nikuombe mtoto yule apelekwe Hospitali ya Rufaa ya Mkoa watampa rufaa kwenda Kanda na Kanda watampeleka Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete na mimi mwenyewe nitahakikisha anapata matibabu bure kwa sababu sera inataka mtoto mwenye umri wa chini ya miaka mitano kupata matibabu bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, amewekeza sana kuhakikisha huduma za matibabu ya kibingwa zinapatikana ndani ya nchi. Mwaka jana wagonjwa zaidi ya 167 tulikuwa tunawapeleka nje ya nchi mwaka 2015, mwaka 2017 ni wagonjwa wawili tu, wagonjwa wote wanafanyiwa upasuaji ndani ya nchi. Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bima ya afya kwa wazee; tumetoa maelekezo kwa Halmashauri zote kuwapatia wazee vitambulisho vya matibabu ikiwa ni hatua ya awali kuelekea bima ya afya kwa kila mtu. Tunategemea ndani ya Bunge lijalo tunakuja kwenye Bunge lako tukufu kuleta muswada wa sheria ambao itafanya bima ya afya kuwa ni lazima na wazee wote wenye stahili tutawapa bima za afya bure ili waweze kupata huduma za matibabu bila kikwazo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shaabani Shekilindi swali la nyongeza.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kuniona. Katika Wilaya ya Lushoto kumekuwa na watu wengi wenye magonjwa sugu hasa kwa wale waishio vijijini.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuwapatia dawa wagonjwa sugu hasa wale wenye magonjwa sugu pamoja

na wale wenye mahitaji maalum hasa kwa wale waishio vijijini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Shekilindi, Mbunge wa Lushoto al-maarufu Bosnia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunao wagonjwa wa magonjwa sugu katika Halmashauri zetu mbalimbali lakini nataka kurudia kwamba gharama za magonjwa sugu haya ni kubwa sana kwa sababu mtu anatakiwa kutumia kila siku akianza kutumia. Kwa hiyo, rai yangu ni kwamba tutajitahidi kadri inavyowezekana kuhakikisha dawa hizi zinapatikana ikiwemo dawa za kisukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, suluhisho la kudumu ni kuwahimiza wananchi kujiunga na mifuko ya bima ya afya. Tumeanzisha bima ya afya tunaita ya Kikoa shilingi 76,400 unapata matibabu mwaka mzima mpaka Hospitali ya Rufaa ya Taifa na Hospitali za Kanda. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Watanzania kuwa na utamaduni wa kulipia matibabu kabla ya kuugua kwa sababu wananchi wengi wanakuwa maskini kwa sababu wakiumwa inabidi wauze ardhi ama baiskeli, bima ya afya ndiyo suluhisho. Tutajitahidi kuongeza bajeti ya dawa, lakini pia kwa mujibu wa sera lazima wananchi wachangie huduma za afya. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri mtusaidie kwa sababu ile bima ya afya ya mtu mmoja ya shilingi 76,000 hivi inataka yule mtu alipe fedha zile kwa mkupuo ili aweze kupata matibabu. Sasa ile fedha ni kubwa kwa mtu wa kijijini kuweza kulipa yote kwa pamoja, mtusaidie utaratibu ambao ataweza yeye kuchangia kama wengine wanavyochangia kila mwezi ili mchango wake uwe ni kidogo kidogo, lakini aweze kupata matibabu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Igunga sasa aulize swali lake.

Na. 79

Changamoto Zinazowakabili Wakulima wa Pamba Nchini

MHE.DKT. DALALY P. KAFUMU aliuliza:-

Mwaka 2017 Serikali iliamua kulifufua zao la pamba lililokuwa limekufa lakini licha ya wakulima wa pamba kuitikia wito wa kulima pamba kuanzia msimu wa mwaka 2018, bado wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo kuchelewa kupelekewa pembejeo kama viuatilifu, kupelekewa viuatilifu visivyoya wadudu, bei ndogo ya pamba, kuuziwa mbegu kwa mikopo yenye riba kubwa.

(a) Je, ni lini Serikali itazishughulikia changamoto hizo ili kukuza ari ya wakulima kulima pamba kwa wingi?

(b) Je, ni kwa nini wakulima wasipewe mbegu bure kama ilivyokuwa zamani ili kuondoa usumbufu wa kukopeshwa na wanaposhindwa kulipa wanakamatwa na kuteswa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mbunge wa Jimbo la Igunga lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya changamoto za wakulima wa pamba katika kuongeza tija na uzalishaji ni upatikanaji wa pembejeo kwa wakati, wakulima kutotumia kikamilifu pembejeo na uzingatiaji wa

kanuni za kilimo bora cha zao la pamba. Aidha, Serikali imeendelea kudhibiti ubora wa pembejeo kupitia mamlaka mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi ya *TPRI* na Mamlaka ya Udhhibiti wa Ubora Mbegu (*TOSCI*) kwa kufanya majaribio (*germination tests*) ya mbegu za pamba kabla ya kupeleka kwa wakulima kwa ajili ya kupanda pamoja na kuainisha maeneo ya Meatu na Igunga kama maeneo ya kuzalisha mbegu za pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeelekeza wakulima wote kuanzia msimu wa mwaka 2018/2019 kutumia mbegu aina ya UKM08 na iliyoondolewa manyoya (*delinted seeds*). Aidha, kutokana na mikakati hiyo, uzalishaji wa pamba umeongezeka kwa asilimia 67 kutoka tani 133,000 msimu wa ununuzi wa 2017/2018 hadi tani 221,600 msimu wa 2018/2019.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuweka mazingira wezeshi ili wakulima waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kupata faida ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya kuendeleza kilimo ikiwemo ununuzi wa pembejeo. Katika kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo, Halmashauri ya Wilaya ya Igunga ilidhamini mkopo kwa wakulima kwa kutumia ushuru wake unaotokana na pamba ambapo wakulima walipata fursa ya kukopa mbegu msimu uliopita na hadi mwezi Oktoba, 2018 wamarejesha shilingi 1,293,997,400 kati ya shilingi 1,567,698,000 zilizokopeshwa sawa na asilimia 82.5. Aidha, utaratibu wa zamani haukuwa kuwapatia wakulima mbegu bure bali wakulima wa pamba waliwekewa utaratibu wa kukopeshwa kupitia Vyama Vikuu vya Ushirika na vya Msingi na kukatwa wakati wa kuuza pamba yao. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Dalaly Peter Kafumu swali la yongeza.

MHE. DALALY P. KAFUMU: Mheshimiwa Naibu Spika, asante sana. Nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba sasa niulize maswali mawili ya yongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, wakulima kwenye msimu wa mwaka 2017/2018 hawakupata mavuno tarajiwa kwa sababu walipata viuatilifu ambavyo havikuu wadudu, lakini pia mvua ilikuwa kubwa sana, kwa hiyo, pamba ikarefuka sana. Kwa nini sasa Serikali isiamue kuhamisha deni la mbegu kwenda msimu unaokuja kwa wale ambao wameshindwa kulipa kwa sababu ya kushindwa kupata mazao ya kutosha?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka nikiwa kijana miaka ya 1960 mpaka 1980 nilikuwa nalima pamba kwa ajili ya kujilipia ada na tulikuwa tunaenda kwenye *godown* la pamba la ushirika tunachukua mbegu na tunalima, hatukuwa na mikataba yoyote. Kwa nini sasa Serikali isirudishe utaratibu huo tuweze kupata mbegu wakulima tukalima bila kusumbuliwa kama tunavyofanyiwa sasa kiasi kwamba tunapelekwa jela na tunatishwa? Nakushukuru. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Niabu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi lakini kama alivyoeleza kwenye swali lake la nyongeza kwamba uzalishaji uliathirika kwa wakulima wengi kutokana na viuatilifu anasema hafifu, lakini pamoja na mabadiliko ya tabianchi kutokana na mvua kubwa iliyonyesha na ombi lake la kusema kwamba tuhamishe deni hili mpaka msimu ujao, kwanza ushauri wake tunaupokea lakini kwamba jambo hili linahitaji tufanye tathmini ya kina na kufanya uhakiki ili tubaini ni wakulima gani ambao walipata na wakulima gani ambao hawajapata. Baada ya uhakiki huo ndio tutaweza kutoa maamuzi kama Serikali nani ambaye asamehewe mpaka mwakani na nani anastahili kulipa kwa sababu dawa ya deni ni kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, utaratibu wa kuwapatia mikopo au mbegu kama utaratibu wa zamani. Huo ushauri wake tunauchukua lakini kama anavyofahamu, hivi Vyama vya Msingi vya Ushirika (*AMCOS*) pamoja na

unions, zile Ushirika Mkuu vilikufa, kama Serikali ndiyo tuko kwenye mkakati mkubwa wa kuweza kuvifufua nchi nzima ili baadae vikishakuwa vimeshahimili na kupata uzoefu tutaweza kurudisha majukumu hayo kwao, lakini kwa sasa lazima kama Serikali tuweze kusimamia kwa sababu bado vyama hivi ni vichanga, twende kwa utaratibu uliokuwepo mpaka hapo vyama hivi vitakapoimarika.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hadji Mponda swali la nyongeza.

MHE. DKT. HADJI H. MPONDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Malinyi, Mkoa wa Morogoro ni mojawapo ya Wilaya zinazolima zao la pamba. Sasa hivi karibu miaka mitatu zao hilo linaathirika na panya waharibifu wanaokula mbegu za pamba mashambani, msimu wa kilimo karibu unakaribia (Desemba), maana yake mwezi ujao.

Swali langu je, Serikali ni lini wataleta viuatilifu (sumu ya kuaa panya hao) vya kutosha na kwa wakati muafaka? Nakushukuru.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kweli, hasa Kanda ya Mashariki iliathirika sana na athari ya wanyama hawa panya, wadudu panya, kuharibu mazao wakati wa kupanda. Lakini nimwambie kwamba kama Serikali, mimi binafsi au kwa niaba ya Serikali, tulishatembelea katika kituo chetu cha kudhibiti panya na kwa bahati nzuri kipo palepale Morogoro, Mkoani kwake na tulishawapa maelekezo kwa sababu mfumo wa Serikali pesa tulikuwa tunawapelekea kwa bajeti, lakini kwa kuzingatia msimu wa kilimo mwaka huu tumejipanga kwamba pesa zote kwa mujibu zinahitajika kwenye sekta ya

kilimo ziende kabla ya msimu ili zisipishane na msimu wa kilimo, ziende kutekeleza lengo lililokusudiwa.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwaka huu Serikali imejipanga na pesa hizi za viuatilifu kuhusu wadudu wa panya zitaenda kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pascal Haonga swali la nyongeza.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazolikabili zao la pamba zinafanana kabisa na changamoto za zao la kahawa. Katika Kijiji cha Mbimba, Wilaya ya Mbozi kuna Kituo cha Utafiti cha *TaCRI* ambacho kinafanya utafiti wa magonjwa ya zao la kahawa pamoja na mbegu za zao la kahawa. Lakini kituo hiki cha *TaCRI* hakijapelekewa fedha kwa muda mrefu sana ili kiendeele kufanya utafiti wa mbegu bora ya kahawa.

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka fedha kwenye kituo hiki cha *TaCRI*/kilichopo Mbozi ili kiendeele kufanya kazi vizuri kabisa, kufanya utafiti pamoja na kupeleka mbegu kwa wakulima wa zao la kahawa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Wilaya ya Mbozi tuna Kituo chetu cha *TaCRI* ambacho ni Kituo cha Utafiti cha Zao la Kahawa, na kituo hiki kinapata bajeti yake kupitia sehemu mbili ambao ni kupitia Serikalini na sehemu kupitia wadau wengine wa maendeleo, sisi kama upande wa Serikali, kama unakumbuka mwaka jana tulileta sheria hapa na ikapitishwa na Bunge lako, Sheria Na. 10 ya *TARI* kwa vituo vyote vya utafiti kuwa katika mwavuli mmoja na baada ya hapo kila kimoja kitapelekewa pesa kutokana na bajeti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka huu, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba baada ya kujua mahitaji hayo ya Sekta ya Kilimo kama Serikali pamoja na Kituo hiki cha *TaCRI* tutakipelekea fedha kwa mujibu wa bajeti yao na kwa wakati.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa swali la nyongeza.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la msingi linazungumzia kuhusu changamoto za zao la pamba, lakini kuhusu viuatilifu ni kwamba vinaletwa ambavyo havina viwango na ndiyo maana inasababisha wadudu kutokufa.

Swali langu, je, ni lini sasa uchakachuaji huu wa madawa ya kuaa wadudu wa pamba utaisha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu kwa swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hayo malalamiko yapo, siyo Mwanza tu au Kanda ya Ziwa, ni sehemu kubwa ya wanaolima pamba, kwamba kuna viuatilifu ambavyo vimeonekana kwamba haviui hao wadudu wa pamba, lakini sisi kama Serikali baada ya kupata tatizo hili tuliwatuma wataalam wetu kwenda kufanya uhakiki na tathmini kama yale yanayosemwa ni kweli. Wataalam hawa walivyokwenda huko wamethibitisha mbele ya wakulima sehemu zingine kwamba imegundulika kwamba ni matumizi hafifu au uelewa mdogo wa baadhi ya wakulima walionao wa jinsi ya kutumia yale madawa kwa sababu wale wataalam waliwathibitishia mbele yao yalionekana kwamba yale madawa yanaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, nitoe wito kwa wakulima; kwa sababu tuna Taasisi yetu ya Udhubiti wa Viuatilifu na Madawa yote kwa maana ya *TOSCI*, kwa yeyote

ambaye anaona kwamba ile dawa haijaua waweke *counter sample* ili dawa ile kama imeonekana na imethibitishwa haiui tuirudishe kwa wataalam na ikithibitishwa basi wale wakulima watafidiwa na hiyo kampuni ambayo imesambaza mbegu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ila nimhakikishie mwaka huu Taasisi yetu ya *TPRA* iko vizuri na zingine kwa ajili ya udhibiti wa viuatilifu hivyo, hili tatizo halitatokea tena.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuweza kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali la msingi hapa linalozungumziwa ni tatizo la pamba. Zao la pamba limewakumba matatizo makubwa sana kwa wakulima, viuatilifu vimekuwa ni moja ya matatizo, lakini kuna pamba wananchi walipanda ikakua kama miti badala ya kuwa pamba ya kawaida. Sijui ni kwa nini sasa Serikali na hasa kupitia Wizara hii ya Kilimo, mnafikiri mtafanya nini kuwapa stahili wakulima hawa ambao wamepata hasara sana katika msimu huu ambao umekwisha?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu.

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA): Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la msingi anataka kujua kwamba Serikali tutafanya nini kuwalipa fidia wakulima ambao wamepata madhara ama ya mbolea feki au kutokana na pamba kukua bila kutoa matunda. Kama nilivyosema kwenye jibu la awali, jambo hili hatuwezi kuchukua kwa ujumla wake, ni vizuri kwanza timu ikaenda ikafanya tathmini na ikafanya uhakiki ili tupate wale walioathirika zaidi, tukibaini hao walioathirika *then* Serikali tutajua nini cha kufanya.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa sasa aulize swali lake.

Na. 80

Tatizo la Mawasiliano ya Simu

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA aliuliza:-

Kumekuwa na tatizo kubwa la mawasiliano ya simu kwenye Tarafa ya Mwambao, Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe, eneo hili lina urefu wa kilometa 150 na lina vijiji visivyopungua 22.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo ambayo pia ni ya kiulnzi na nchi jirani na ni tarafa pekee ambayo haina mawasiliano ya simu kabisa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nitoe shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniokoa na ajali mbaya kabisa iliyotokea juzi jioni, saa kumi baada ya gari niliyokuwa nikitumia kupinduka kama mara tano, lakini Mungu ametusaidia tumetoka salama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata nafasi ya kunitumia *message*, hata kunipigia simu kwa ajili ya kunipa pole, ninawashukuru hata wananchi wa jimboni kwangu ambao walipata nafasi ya kunipigia simu au kunitumia salamu, namshukuru Mungu naendelea vizuri, afya yangu iko salama kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nimshukuru sana Mheshimiwa Ndassa ambaye baada ya dakika tano tu alifika eneo la ajali akiwa njiani naye kuelekea huku Dodoma ambaye vilevile aliweza kunipa lifti mpaka kufika Dodoma salama na kunipeleka hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa huduma ya mawasiliano katika maeneo ya mipakani mwa nchi yetu hususan katika kuimarisha ulinzi na usalama. Hivyo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ilizianisha kata nne za Tarafa ya Mwambao na kuziingiza katika zabuni iliyotangazwa mwezi Februari, 2017 na Kata hizo ni Lumbila, Kilondo, Makonde na Lupingu. Kazi ya ujenzi ilitolewa kwa Kampuni ya Simu ya Viettel (Halotel) ambayo ilishinda zabuni na huduma ya mawasiliano inategemewa kupatikana kuanzia mwishoni mwa mwezi huu wa Novemba.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Deogratias Ngalawa swali la nyongeza.

MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kuishukuru Serikali kwamba hizo kata ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amezitaja, kwa maana ya Kata za Lupingu, Makonde, Lumbila na Kilondo, tayari mkandarasi yupo kazini. Sasa ninachopenda kuuliza ni kuwa je, ni lini minara hiyo itawashwa; kwa sababu baadhi ya minara tayari imeshajengwa lakini kuwashwa bado, ni lini itawashwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuna baadhi ya maeneo ambayo tayari tuliomba mfano Kata ya Ludende,

Kata ya Lupanga na Kata ya Iwela, ni lini Serikali itatufikiria kwenda kujenga tena mawasiliano mengine?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Deogratius Ngalawa kwa sababu bahati nzuri nimekwishafanya naye ziara kwenye Jimbo lake la Ludewa, hasa Kata ya Mwambao ambako tulitembelea maeneo ya Lupingu, Vijiji vya Nindi, Mtumbatu; lakini tulitembelea Kata ya Makonde kwenye Vijiji vya Manyanya na Liunji; vilevile tulitembelea Kata ya Kilondo kwenye Vijiji vya Kilondo Kijinini na Nsele na kuona changamoto za mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini na yeye mwenyewe amekiri kwamba tayari kuna baadhi ya minara imeshawekwa, tulikuwa bado tuna changamoto ya *battery* kwa sababu maeneo yale Mheshimiwa Mbunge anaendelea kufanya jitihada ya kuhakikisha kwamba umeme wa *REA* unafika na sisi kwa sababu tunahitaji watu wawasiliane tuliweka *system* ya *solar* ambayo betri zake zilikuwa zina changamoto kidogo na sasa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba *battery* zimekwishafika na ndiyo maana nimezungumza kwa uhakika kwamba inapofika mwishoni mwa mwezi huu basi tutakwenda kuwasha hiyo minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu Kata za Iwela, Lupanga na Ludende, kuna orodha ambayo tunaendelea kuiandaa ambayo mwisho wa mwezi huu tunategemea tutakuwa na kata zaidi ya 206 ambazo tutakwenda kuziweka kwenye programu ya kuwapatia mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nakushauri itakapofika kipindi hicho uje tuwasiliane ofisini ili uangalie kama vijiji vyako kwenye kata hizo vitakuwa vimewekwa. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zuberi Kuchauka swali la nyongeza.

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Liwale yenye kata 20 ni kata tano tu zinafikika kwa mawasiliano ya simu. Nini kauli ya Serikali ili kuwapatia wananchi wa Kata za Mirui, Mkutano, Mtungunyu, Lilombe, Ngongowele, Mpigamiti pamoja na Mlemwe ili waweze kupata mawasiliano ya simu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna changamoto kubwa sana ya mawasiliano katika Jimbo la Liwale na hivi karibuni nilituma timu yangu ya wataalam kutoka *TCRA* na *UCSAF* kwenda kukagua maeneo hayo ambapo tayari nasubiri taarifa hivi karibuni, zitakapokuja tunategemea kwenye hizi kata 203 tunazotegemea kuzitangaza na wao watakuwepo. Tuna nia ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mawasiliano nchi nzima kuhakikisha kwamba usalama na uchumi wao unalindwa ipasavyo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rashid Shangazi swali la nyongeza.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa mawasiliano katika Kata ya Malindi, Kijiji cha Makose na katika Kijiji cha Chagoka Kata ya Rangwi, lakini pia katika Kijiji Longoi eneo la Bustani

yatakamilika kwa sababu ndiyo maeneo pekee ambayo yamebaki katika Jimbo la Mlalo, Halmashauri ya Lushoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Vijiji vya Makose, Kata za Langoi, Bustani na Kinko pamoja na Goka mawasiliano ni hafifu sana. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kufanya uchambuzi kuhakikisha kwamba minara iliyopo jiani kwanza inaongezewa nguvu kuweza ku-*cover* eneo kubwa sana la mawasiliano; lakini pili, tumeendelea kuyaainisha maeneo ambayo hayataweza kufikiwa na *improvement* ya minara hiyo kuanza kuweka minara mipya.

Namshauri Mheshimiwa Mbunge tuendeleo kuwasiliana kwa sababu mara nyingi kwa kweli nampongeza kwa jinsi anavyofuatilia suala la mawasiliano kwa wananchi wake. Tuendeleo kuwasiliana naye ili kuona vijiji ambavyo havitafikiwa baada ya kupata ripoti ya watu wa *TCRA* na *UCSAF* tuweze kuviingiza kwenye mpango ambao mwisho wa mwezi huu tutatangaza hizo orodha za kata na vijiji vitakavyowekewa mawasiliano.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwita Getere swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nimpe pole ndugu yangu, Mheshimiwa *Engineer* Nditiye na kwa sababu humu ndani kuna bibi, kuna mke wa Chifu Makongoro ana miaka 100 na amekuona atakuomba ndugu yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza swali, Serikali imekuwa ikiahidi kujenga minara katika Vijiji vya Nyangere, Nyaburundu, Tiling'ati na Jabuzunde kwa muda mrefu sasa. Sasa ni lini ahadi ya Serikali itatekelezwa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna changamoto katika Vijiji vya Nyandetere na Timati na maeneo kadhaa ambayo ameyaruka kidogo, lakini nimuahidi tu Mheshimiwa Getere kwamba mwezi ujao tutakuwa wote jimboni kwake kwa ajili ya kuchunguza maeneo mengi zaidi tuhakikishe kwamba wananchi wa jimbo lake wanapata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania wote kwa ujumla, kwamba tunapoelekea uchumi wa kati ambao ni wa viwanda mwaka 2025, tumeona jinsi ambavyo wananchi wanahitaji mawasiliano kiuchumi na kiusalama na ndiyo maana sasa hivi huwezi kusikia tu changamoto za maji, barabara, umeme bila kusikia changamoto za mawasiliano, ni kwa sababu kila mwananchi sasa hivi (asilimia 94) anamiliki simu za mkononi na anahitaji mawasiliano na sisi kama Serikali tuendeleo kuwahakikishia wananchi kwamba tumejipanga kuhakikisha kwamba kabla ya mwezi Machi mwakani tutakuwa na asilimia 99 ya wananchi wote ambao wanawasiliana ili kufanya kwamba shughuli zao za kiuchumi ziwe imara na usalama wao uimarike zaidi.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Vedasto Ngombale swali la nyongeza.

MHE. VEDASTO E. NGOMBALE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini Serikali itajenga minara ya mawasiliano katika Vijiji vya Mtumbei, Mpopera, Kandawale, Kibata, Nandete na Kinjumbi?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kuorodhesha maeneo mbalimbali ya nchi yetu ambayo hayana mawasiliano na vijiji ulivyovitaja Mheshimiwa nina hakika vimo, lakini kwa uhakika zaidi, kama hutajali, upate nafasi uje ofisini ili ujiridhishe mwenyewe kwenye *database* yetu kwamba vijiji ulivyovitaja vimo na vitatangazwa kabla ya mwezi huu kuisha kuhakikisha kwamba tunapeleka mawasiliano maeneo hayo. Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia.

Na. 81

Hitaji la Kivuko Maalum Kilindoni na Nyamisati

MHE. MBARAKA K. DAU aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga kivuko maalum (*landing craft*) kwa usafiri wa Kilindoni (Mafia) na Nyamisati (Kibiti)?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau Mbunge wa Mafia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) katika mpango wa bajeti wa mwaka 2018/2019 imepanga kunua Kivuko kwa ajili ya usafiri wa majini katika bahari ya Hindi kati ya Nyamisati na kilindoni Mafia Mkoani Pwani ili kutoa huduma salama ya kuvusha abiria na mizigo na hivyo, kukuza uchumi wa wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ufundi na Umeme umeanza taratibu za ununuzi wa kivuko hiki ambako zabuni kwa ajili ya ununuzi wa nkivuko hicho kipya kitakachokuwa na uwezo wa kubeba uzito wa tani 100 sawa na abiria 200 na magari madogo sita imetangazwa tarehe 24 Oktoba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandara (TPA) mwaka 2013 ilikamilisha ujenzi wa gati katika eneo la Kilindoni, Kisiwani Mafia. Kwa sasa Wizara inaendelea na ujenzi wa gati upande wa Nyamisati Wilayani Kibiti pamoja na miundombinu mingine yaani nyumba na ofisi ya Mhandisi, jengo la mizigo na abiria na maliwato. Mradi huu ambao utatekelezwana Mkandarasi *Alpha Logistics and Southern Engineering Company JV* kwa gharama ya shilingi 14,434,673,467 ulianza tarehe 16 March, 2018 na umepangwa kukamilika ndani ya muda wa miezi 12.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya ujenzi wa Gati ya Nyamisati pamoja na ujenzi wa miundombinu mingine katika eneo hilo hadi sasa umefikia kiasi cha 35% na mkandarasi ameshalipwa kiasi cha shilingi 1,373,073,256.71.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau swali la nyongeza.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inakiri boti hii itakuwa tayari baada ya mwaka mmoja; na kwa kuwa katika kipindi chote hicho wananchi wa Mafia wataendelea kutumia vyombo hatarishi vya baharini vilivyojengwa kwa magogo; na kwa kuwa Serikali imeshasema kwamba boti hii itakamilika ifikapo mwaka 2019; na kwa kuwa mfanyabiashara maarufu Bakharesa ametoa boti bure kwa Serikali ambayo hivi sasa inamaliziwa matengenezo; na kwa kuwa wataalam wa *DMI* ambao wamekabidhiwa boti hiyo wameshakuja Mafia na wamejiridhisha na miundombinu na

kupanga nauli kinachosubilika sasa ni Mheshimiwa sana Waziri mwenye dhamana kuridhia tu boti ile ije Mafia na kuanza kutoa huduma.

Je, ni lini sasa Mheshimiwa Waziri ataridhia boti ile iliyotolewa na mfanyabiashara Bakharesa ije Mafia na ianze kutoa huduma? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mheshimiwa Naibu Waziri Gati la Kilindoni lipo katika hali mbaya sana, mbao zimechakaa, ngazi imechakaa na pepo za Kaskazi zinataraiza kuanza wakati wowote hivi sasa.

Je, ni lini sasa Wizara itaiagiza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* kufanya ukarabati mkubwa wa Gati la Kilindoni ili likidhi hadhi ya kuchukua abiria? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu, Mheshimiwa Nditije.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano napenda kwanza kumpongeza Naibu Waziri mwenzangu kwa majibu yake mazuri lakini naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Dau maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba tulikuwa na kikao kirefu sana kati ya Mheshimiwa Mbaraka Dau ambaye anafuatilia sana changamoto za usafiri wa majini kwa wananchi wake, lakini tulikuwa na watu wa *DMI* na pia tukawa na watu wa bandari katika kuhakikisha kwamba hiyo meli ambayo *DMI* walipewa na Bakharesa inaweza kuanza kufanya kazi na *process* zote ambazo tulikuwa nazo mimi na Mheshimiwa Mbaraka Dau anazijua, tulifanya kikao na tukakubaliana sasa ile boti ianze kufanya *sea test*. Siku ambayo tulikuwa tumekubaliana ifanye *sea test* kukawa na hali mbaya ya hewa ambako boti nyingi sana

hata Zanzibar hazikuweza kwenda, tukaahirisha kwa ajili ya kufanya siku nyingie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali bado ina nia ya kuwasaidia wananchi wa Mafia kwa dharura hiyo kwa sababu mpango endelevu ni wa kutengeneza kivuko kikubwa, lakini hivi karibuni tutaanya tena *sea test* halafu tutapanga namna ya kuanza safari za kutoka Mafia mpaka Dar es Salaam Mjini katikati.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuna wataalam ambao tumeshawatuma kutoka bandari Mamlaka ya bandari kwa ajili ya kwenda kufanya tathimini na ripoti imekwishakuwa tayari tunaangalia namna sasa ya kuanza kutafuta mkandarasi wa kurekebisha hiyo Gati ya Kilindoni ambayo ni muhimu sana kwa wananchi wa Mafia. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Dkt. Charles Tizeba Mbunge wa Buchosa. *(Makofi)*

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, lakini kabla sijauliza swali hilo niruhusu niseme maneno mawili tu, la kwanza ni kumshukuru Mheshimiwa Rais, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa fursa aliyokuwa amenipa ya kulitumikia Taifa. Pia nikushukuru wewe na Mheshimiwa Spika kwa ushirikiano nilioupata wakati nikitumika Serikalini ndani ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naswali dogo la nyongeza, kwamba Jimbo langu la Buchosa linavyo visiwa zaidi ya 28 na katika Visiwa hivi 28 kuna vivuko viwili kivuko kimoja kimepitwa na wakati kinakuwa *overloaded* na watu wakati mwingine wnaogopa hata kukipanda, hili jambo Mheshimiwa Naibu Waziri Kwandikwa analifahamu vizuri, ninachoomba kujua, je, *commitment* ya kujenga kivuko kipya kati ya Nyakalilo na Kome bado iko palepale au la? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kwandikwa inavyoonekana majibu ya swali hili yanasubiriwa na Bunge zima kwa namna ya Mheshimiwa alivyopokelewa humu ndani.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nimshukuru Mungu kupata nafasi ya kujibu swali la Mheshimiwa Tizeba ambalo limepigwiwa makofi mengi sana. Lakini maalum nimshukuru Mheshimiwa Tizeba kwa sababu tulitembelea Jimboni kwake, tulitembelea Kivuko cha Nyakalilo na nilijionea shida wananchi wanayopata kuvuka kwenda kule Kisiwani. Lakini pia nilishuhudia juhudi Mheshimiwa Mbunge alifanya ili kuhakikisha kunakuwa na uchumi, kuna shughuli za uvuvi, kuna kilimo cha misitu kule, fursa ziko nyingi lakini kikwazo pia ni usafiri wa kuvuka kwenda kule visiwani.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Buchosa kwamba tumeunda timu maalum ambayo inatembelea maenewo yote ya vivuko na itawasilisha taarifa kwa ajili kuboresha kuangalia namna nzuri ya kuendelea vivuko vyetu. Na katika eneo hilo la Nyakalilo tuliona namna jinsi ambavyo watu kupanda tu kwenye kivuko mpaka wanagombana wanapigana hadi ngumi kwa sababu ya uwezo mdogo wa kivuko ulichokuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Tizeba nikuhakikishie ni kwamba tutabadilisha kile kivuko utaratibu unaendelea vizuri na nitaendelea kukupa mrejesho hatua ya haraka ambayo tunaifanya ili tuweze kuboresha usafiri wa kwenda Buchosa, lakini ili tuweze kwenda sambamba na mahitaji ya ongezeko la watu na huduma za kijamii ambazo ziko katika eneo lako Mheshimiwa Tizeba. Nashukuru.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa.

Na. 82

Barabara ya Mbalizi - Makongolosi

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. PHILLIPO A. MULUGO) aliuliza:-

Serikali kupitia *TANROADS* walishafanya upembuzi yakinifu kwenye barabara ya Mbalizi - Makongolosi toka mwaka 2013 lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea.

Je, ni lini Serikali itaanza kuweka lami barabara hiyo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI, UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philipo Augustine Mulugo Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mbalizi hadi Makongolosi ni barabara ya Mkoa yenye urefu wa kilometa 116.98 ambayo inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya kwa kuwa inapita Makao Makuu ya Wilaya ya Songwe kwa kupitia Mbalizi Mkoa wa Mbeya na inapita katika machimbo ya madini ya Shanta eneo la Saza lililoko Wilayani Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa kwa kutambua umuhimu wa barabara hii Serikali imefanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami sehemu ya Mbalizi hadi Galula yenye urefu wa kilometa 56 na Serikali imekuwa ikitenga fedha kila

mwaka kupitia *TANROADS* Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya kwa ajili ya kuifanyia matengenezo ya aina mbalimbali ili iweze kupitika majira yote ya mwaka ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilitenga kiasi cha shilingi milioni 553.920 kupitia *TANROADS* Mkoa wa Songwe na kiasi cha shilingi milioni 441.885 kupitia *TANROADS* Mkoa wa Mbeya na katika mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 633.920 kupitia *TANROADS* Mkoa wa Songwe na kiasi cha shilingi milioni 730.778 kupitia *TANROADS* Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara iliyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kuanzia Mbalizi hadi Galula kilometa 56.0 na kwa ajili ya kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina sehemu ya barabara iliyobaki ya kuanzia Galula - Mkwajuni hadi Makongolosi kilometa 61.

NAIBU SPIKA:Mheshimiwa Victor Mwambalaswa swali la nyongeza.

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

La kwanza sasa hivi Bunge lako linakaa kama Kamati ya Mipango tunapanga mpango wa mwaka kesho bajeti 2019/2020 na hii barabara ya Mbalizi - Makongolosi ni barabara ambayo inaunganisha mikoa miwili Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya na Serikali imesema imefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara hi kutoka Mbalizi mpaka Galula.

Je, kwenye bajeti ijayo Serikali itatenga fedha kidogo ili barabara hii ianze kujengwa kwa lami kidogo kidogo? La kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili hii barabara ikifika pale Makongolosi inakuta na barabara inayotoka Mbeya - Chunya - Makongolosi kwenda Rungwa. Hasa barabara hiyo kutoka Chunya kwenda Makongolosi inajengwa kwa lami sasa hivi na imepata mkandarasi ambaye yuko kazini. Mheshimiwa Waziri alipita mwezi wa nane akamkuta huyu mkandarasi kwanza ana vifaa vichache, pili kasi yake ni ndogo.

Je, Serikali inachukua hatua gani kurekebisha huyu mkandarasi ili ajenge katika mkataba ambao tulikuwa tumesainiana naye? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba tuna fedha zikipatikana mara moja tutaaanza kujenga hii barabara kama nilivyosema katika jibu langu la msingi. Kwa hiyo tukipata fedha tuaanza ujenzi wa barabara hii. Lakini pia niseme tu kwamba mimi wkeli nilitembelea barabara hii na maeneo yote ambayo yalikuwa korofi tayari yalikuwa yameshawekewa klipande cha lami muda mrefu na kipande hichi kimechoka kwa hiyo umuhimu wa kujenga barabara hii upo tutajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu barabara hii ya Makongolosi hadi Chunya kweli ni kilometa chache kutoka upande wa Songwe zitaunganika na hii barabara ambayo tunajenga kiwango cha lami upande huu wa Chunya. Lakini kasi kweli ilikuwa ndogo na mimi nilifika eneo la mkandarasi huyu lakini tu nimfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Mheshimiwa Waziri alishachukua hatua tayari za kuhakikisha kwamba ujenzi huu unachukua kasi yake kama Serikali tunavyotegemea, na mkandarasi kama unavyojua Mheshimiwa Mbunge wale wataalam waliokuwepo tuliona kwamba wana mapungufu na Mheshimiwa Waziri alielekeza wale waondolewe ili tupate wataalam ambao mkandarasi atawatumia kuhakikisha

kwamba ile kasi ambayo tunaitegemea kama Serikali kwamba tunaipata lakini pia tunapata ubora lakini wananchi wanahitaji kwa muda mfupi waweze kutumia barabara hii, kwa hiyo hatua tayari imeshachukuliwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Innocent Bilakwate swali la nyongeza.

MHE. INNOCENT S. BILAKWATE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza, barabara ya kutoka Mgakolongo kwenda Kigalama, Ugomola mpaka Mlongo ni ahadi ambayo imehaidiwa muda mfrefu na barabara hii bado haijatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kujua ni lini barabara itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuondoa kero ambayo iko kwa wananchi wetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli harakati za ujenzi wa barabara hii kutoka Mgakolongo - Kigalama hadi Mulongo tulishaanza usanifu na tulikuwa tupo kwenye hatua za mwisho. Mara ya baada ya usanifu wa barabara hii Mheshimiwa Bilakwate na wananchi wa Kyelwa na maeneo ya Jimbo la Karagwe niwahakikishie tu kwamba tutaanza kujenga kwa sababu utaona kwamba liko hitaji eneo hili la Mulongo ni eneo ambalo lina miteremko mikali sana, ni hatari, lakini utaona ule upande wa wenzetu upande wa Uganda wameshatengeza barabara tayari kwa sababu ya mkakati ule wa kuunganisha nchi yetu na nchi jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo umuhimu wa kufanya ujenzi wa barabara hii pia tutaanza hivi karibuni kupanua daraja hili la Mulongo, kwa sababu daraja lile lina muda mfrefu na lilitengenezwa kwa teknolojia ya zamani, kwa hiyo ule utaratibu wa kutengeneza daraja hili katika eneo hili la

Mulongo Mheshimiwa Mbunge nikufahamishe pamoja na wananchi kwamba tunaanza kulipanua daraja hili, lakini tutakapokamilisha usanifu wetu ujenzi wa barabara hii muhimu kilometa utaanza kujengwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Oran Njeza swali la nyongeza.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa na mimi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyokuwa umuhimu wa barabara ya Mbalizi - Makongolosi vilevile kuna barabara ya kutoka Mbalizi - Shigamba mpaka Isongole ambayo ni muhimu sana kiuchumi na vilevile ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na pia na ahadi ya Mheshimiwa Rais wetu.

Je ni lini hii barabara itajengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anatambua kwamba mimi nilitembelea eneo hili na nafahamu kwamba yako maeneo ambayo ni korofi lakini pia kuna sehemu kubwa ya uzalishaji katika eneo hili. Pia kwa sababu tumeshaanza kujenga barabara ile inayokwenda lleje ni muunganiko mzuri wa wananchi wa maeneo haya, kwa hiyo tunaendelea na harakati za kufanya maandalizi ya awali ili kuhakikisha barabara hii muhimu tunajenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge hii ni ahadi ya viongozi wakuu, awamu ya nne ilikuwa ni ahadi pia kwenye mpango mkakati wa ujenzi wa barabara hii tumeionyesha kwa hiyo nikuombe tu uvute subira yako maboresho ya barabara kwenye eneo lako Mheshimiwa Mbunge ambayo tunayazingatia kwa sababu huko umuhimuwa wakuwaunganisha wananchi wa lleje wakipita

kwenye maeneo ya kwako kwenda upende ule wa Kyela. Kwa hiyo, tunaitazama kwa macho mawili pia itakuwa msaada mkubwa wa kupunguza misongamano ambayo siyo ya lazima katika Jiji la Mbeya. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya swali la nyongeza.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua Serikali ina mkakati wa kujenga hizi barabara za pete kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kuunganisha Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam kwa mfano barabara ya kutoka pale *stand* ya Kibaha unatokea Baobao kabla ya mpakani mwa Dar es Salaam na Bagamoyo lakini na barabara hii ya Makongo - Goba - Kimara.

Sasa nilitaka kujua ni lini hizi barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami kwasababu ni kweli zinapunguza foleni na kusaidia watu wengi ambao wanasafiri kutoka mikoa mbalimbali kuja Dar es Salaam au kutoka Dar es salaam kwenda Dodoma? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ingefaa Mheshimiwa Bulaya labda baadae tunaweza tukakaa kwa sababu ile mikakati ilyopo ni mingi ili niweze kuipata sawasawa nikushauri tu ukipata nafasi tuweze kuzungumza.

Lakini kwa ufupi kabisa niseme kwamba tunaendelea kuhuisha mipango mbalimbali ambayo ipo. Tulikuwa na ule uratibu wa kutengeneza barabara ya njia sita kutoka Mbezi kwenda ule upande wa Pugu, lakini kutoka Mbezi kwenda upande wa Bunju, lakini tumeona kwamba tuitazame sambamba na kuona ule ukuaji ukija huku upande wa

Kibaha, sasa tunatazama hii barabara ya njia sita ili tuje kutoka Kibamba kwenda Bunju na kutoka Kibamba kutafuta uelekeo ule wa kwenda Pugu. Kwa hiyo tunaendelea na usanifu ili kuona *the best way* tunaweza tukazona hizi barabara zinakaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hizi barabara sasa kama tutafanya marekebisho ina maana barabara za kutoka Mbezi zinaweza zisiwe na njia sita zikabakia njia mbili ili kuruhusu sasa ujenzi uje Kibamba wka hiyo bado tunafanya mapitio, ndiyo maana nikushauri tu upate nafasi ili tuweze kuangalia *network* nzima ya Jiji na Dar es Salaam kwa sababu njia sita zitakavyokuwa zinakuja Kibaha bado kutakuwa na mvuto mkubwa sana wa kuyachochea magari mengi yanayotoka katikati ya mji kwamba inaweza ikasababisha tena foleni kwa upande huu. Kwa hiyo tunaitazama kwa macho mawili.

Kwa hiyo nikushauri tuonane ili angalau uipate sawa sawa ili wananchi wanayo nafasi ya kuwajulisha namna nzuri Serikali inafanya ili kuboresha usafiri wa Jiji la Dar es Salaam.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Kiruswa swali la nyongeza.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuruna mimi naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa kuna umhimu mkubwa wa kutengeneza hizi barabara za *bypasses* (za pete), kuna barabara nzuri hi ya kutoka Lingido kwenda Kilimanjaro kupitia Siha na ni moja ya barabara ambazo zimebainishwa katika ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015/2020 na ninaomba kuuliza, je, ni lini sasa mchakato wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami utaanza? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mwasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli upo umuhimu wa kujenga hizi barabara za *bypass* na nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tumezungumza mara nyingi, lakini na mimi pia nilitembelea eneo hili kuona *logistic* za kuunganisha barabara hii ya kwenda Longido. Nilivyotembelea hii barabara, ukitoka Bomang'ombe kuna huu mradi ambao unatoka Lelai kwenda Kamwanga ambao pia utakuwa kiungo kizuri cha hii *bypass* ambayo inakwenda Longido.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie tu kwamba tunaitazama kwa makini barabara hii. Iko ile haja ya kuiunganisha barabara hiyo na kwenye mradi huo wa barabara ambao tutakwenda Kamwanga kwenda kuunga upande ule wa Rombo tutaitaza kwa macho mawili kipande hiki ili kiweze kuunganika na barabara hii muhimu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Makilagi swali la nyongeza

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Musoma - Busekela - Makojo mpaka Bukumi ilifanyiwa upembuzi yakinifu tangu miaka mitatu iliyopita na Mheshimiwa Rais alivyofanya ziara Mkoa wa Mara mwezi mmoja uliopita aliagiza barabara hii ijengwe kwa kiwango cha lami na tender itangazwe mara moja. Ningepanda kujua tangu Rais ametoa maelekezo haya mpaka sasa hatua imefikia wapi ili barabara ya Majita - Busekela - Makojo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

NAIBU WAZIRI UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli

kabisa Mheshimiwa Rais alivyofanya ziara katika mkoa alitoa maelekezo na mimi nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mara kwa ujumla wake kwamba tayari hatua za kutangaza ujenzi wa barabara Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo kwa barabara inayotoka Bunda Mheshimiwa Mbunge umeitaja, kwa hiyo, hii barabara inatangazwa kwa ajili ya ujenzi lakini iko barabara nyingine kwa upande huo wa Mara kutoka kule Nata, Sanzate na yenyewe iko katika hatua ya kutangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nilihakikishie tu Bunge lako na Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais na nimushukuru sana Mheshimiwa Rais anatupa *support* kubwa ili na sisi kama Wizara tuendeleo kutekeleza majukumu ya Wizara kwa umahiri mkubwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Wizata ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 83

Wizi wa Kuvuja kwa Mitihani

MHE. SUSAN A. J. LYIMO aliuliza:-

Wizi wa kuvuja kwa mitihani hapa nchini umekuwa ukijirudia mara kwa mara na kwa ngazi zote.

Je, Serikali ina maelezo gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Susan Anslem Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa elimu yetu ni bora, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuhakikisha kuwa usimamizi na uendeshaji wa mitihani unafuata sheria, kanuni na taratibu zilizopo katika ngazo zote za elimu. Matukio ya udanganyifu katika mitihani au wizi wa maswali ya mitihani yamekuwa yakitokea kenye baadhi ya shule au Halmashauri katika ngazi ya elimu ya sekondari na msingi na wahusika huchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu. Aidha, katika ngazi ya vyo hakuna wizi wa mitihani ulioripotiwa isipokuwa yapo matukio ya udanganyifu na inapotokea hatua huchukuliwa kwa mujibu wa kanuni za mitihani za chuo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imesikitishwa sana na tukio la hivi karibuni la baadhi ya viongozi wa elimu na wakuu wa shule kujihusisha na kusambaza maswali ya mitihani ya kuhitimu darasa la saba katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba kwa lengo la kufanya udanganyifu. Tatizo hilo pia lilitokea katika baadhi ya shule za msingi kwenye Halmashauri za Kondo, Kinondoni, Ubungo, Temeke na Mwanza Jiji. Kufuatia tukio hilo, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Kwanza kufuta matokeo ya mtihani na kurudiwa kwa mtihani huo kwa shule zilizohusika na pili kuwachukulia hatua waliohusika na usambazaji wa maswali ikiwa ni pamoja na kuwasimamisha kazi, kuwavua madaraka na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria ili sheria ichukua mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa mitihani katika ngazo zote za elimu. Aidha, Serikali itaendelea kuchukua hatua kali za kisheria kwa mtu yoyote atakayebainika kujihusisha na vitendo vya wizi na udanganyifu katika mitihani nchini.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri au Wizara kwa ujumla ingeongelea zaidi suala la kuboresha maslahi ya walimu kwa sababu elimu bila walimu haiwezekani. Maswali yangu mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni hasa kwenye Awamu hii ya Tano kumekuwa na utaratibu wa viongozi wa Serikali hususani Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mkoa na kadhalika kuwavua madaraka walimu wakuu wa shule au walimu pale inapobainika kwamba shule zao zimefanya vibaya bila kuangalia mazingira ya kufundishia na ya kujifunzia.

Swali langu, Serikali haioni kwamba hatua kama hizo ni kuwadhalilisha walimu na ni kinyume cha utaratibu wa utumishi na kwa maana hiyo walimu hao wanaweza kuhakikisha kwamba wanafanya njia mbadala za kuiba mitihani ili watito hao wafaulu na ili kuhakikisha kwamba kazi zao zinaendelea, hilo swali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (*EP4R*) kuna kipengele cha kuzawadia wanafunzi au walimu pale wanapofaulisha bila kuangalia mazingira ya shule kwa sababu tunajua shule nyingi zingine zina mwalimu mmoja, nyingine wawili na nyingine 50.

Je, Serikali haioni kwa kufanya hivyo kunapelekea zile shule ambazo labda zina matatizo makubwa ya walimu kuweza nao kufanya mbinu za kuiba kama ambavyo imetokea Chemba ambapo Chemba mwaka jana ilikuwa ya mwisho lakini mwaka huu walitaka kuwa wa kwanza?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba alitegemea nitoe jibu kuhusiana na namna ya kuboresha maslahi ya elimu, siyo swali ambalo Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwahiyoy ilikuwa ni vigumu mimi kwenda kujitayarisha kujibu swali ambalo halijaulizwa.

Lakini kuhusiana na hilo alilosema kwamba kumetokea utaratibu wa Wakuu wa Wilaya kuwavua madaka walimu na kwamba ndiyo anahisi kwamba inahusika na wizi wa mitihani au udanganyifu naomba nimhakikishie kwamba, kwa taarifa ambazo tumezipata, udanganyifu au wizi ambao umetokea hauna uhusiano wowote na hilo ambalo amesema, tumeangalia, tuna ushahidi tunajua kwamba wizi ule umafanyika lakini hauna uhusiano na kuvuliwa madaraka.

Lakini vilevile kuhusiana na kwamba utaratibu wa kuwazawadia wanafunzi waliofaulu kwamba ndiyo unahusika na walimu kujaribu kuiba mitihani, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tunachofanya kama Wizara ni kuhakikisha kwamba hakuna upenyo wowote wa kuiba mitihani kwa sababu ni kinyume na sheria, haijalishi kwamba mtu anaiba mitihani kwa sababu gani, sisi tunachoisema kwamba ni kosa kuiba mitihani na yeyote yule atakepatikana na kosa atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria zilizopo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, walimu wetu wanafanyakazi nzuri sana na wanafanyakazi ngumu sana kwahiyoy tukumbuke kutumia maneno “baadhi” tunapotaka kusema maneno kama hayo kwamba kuna uwezekano wa walimu kuhusika kwenye kuiba mitihani, tukumbuke kutumia maneno “baadhi” kwa sababu walimu wanafanyakazi nzuri sana katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 84

Ongezeko la Vitendo vya Kikatili Shuleni

MHE. ROSE C. TWEVE aliuliza:-

Kumekuwa na ongezeko la vitendo vya kikatili kwenye shule zetu nchini kama vile kuchapa viboko hadi kusababisha vifo.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti au kukomesha adhabu hizi za kutweza (*corporal punishment*)?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose Cyprian Tweve, Mbunge wa viti maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vitendo vya kikatili au unyanyasaji kwa watoto vina madhara makubwa katika makuzi ya kimwili na kiakili. Serikali imeweka mikakati mablimbali kuhakikisha ulinzi wa mtoto dhidi ya ukatili na au unyanyasaji. Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009, kifungu cha 13 inakataza mtu kumsababishia mtoto mateso au aina nyingine ya ukatili, kumpa adhabu zisizo za kibinadamu au kumdhalilisha. Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Adhabu Sura ya 16 ya Sheria za Tanzania kama ilivyorejewa mwaka 2002 ni kosa la jinai kumdhuru, kumjeruhi au kusababisha kifo kwa mtu yeyote na ikithibitika muhusika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Elimu, Sura ya 353 kama ilivyorejewa mwaka 2002, imetoa utaratibu wa namna ya kutoa adhabu ya viboko kwa wanafunzi. Wizara kupitia

Waraka wa Elimu Namba 24 ya mwaka 2002 ilitoa maelekezo na utaratibu wa utekelezaji wa Sheria hii ambapo adhabu ya viboko inaweza kutolewa kwa utovu wa nidhamu uliokitihiri au kwa makosa ya jinai yaliyotendeka shuleni au nje ya shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua kwa wanaobainika kujihusisha na vitendo vya kikatili au unyanyasaji dhidi ya watoto kwa mujibu wa taratibu za kiutumishi na sheria za nchi, kwa mfano; walimu waliohusika kumpiga mwanafunzi wa shule ya msingi Kibeta iliyopo Manispaa ya Bukoba na kusababisha kifo chake walisimamishwa kazi na kufikishwa mahakamani ambapo kesi inaendelea.

Aidha, Afisa Elimu Kata, Mwalimu Mkuu na Msaidizi wake wamesimamishwa kazi kupisha uchunguzi, hivyo nitumie fursa hii kuwataka wasimamizi wa elimu kusimamia kikamilifu utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo ya Serikali. Aidha, napenda pia kuwaasa walimu wote nchini kuepuka vitendo vya kikatili au unyanyasaji kwa watoto.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Rose Tweve swali la nyongeza.

MHE. ROSE C. TWEVE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na mimi nakubaliana kabisa na maelezo yako ya awali kuwa walimu wetu wana mchango mkubwa sana katika malezi na makuzi ya vijana na watoto wetu hapa nchini na sisi wengine tumeweza kufika hapa ni misingi mizuri ambayo tumepewa na walimu wetu.

Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kabisa sheria zetu ziko vizuri, kanuni zetu zipo vizuri lakini kumekuwa na changamoto kubwa katika utekelezaji juu ya utaoji wa adhabu mashuleni. Kwa mfano, sheria inamtaka kabla ya mwalimu hajatoa adhabu lazima apate kibali kwa Mkuu wa Shule na kiasi cha viboko ni viboko vinne, kwa hiyo kama ulivyoonesha Mheshimiwa Waziri kuna baadhi ya walimu wachache ambao wamekuwa na changamoto kubwa ya kufuata taratibu na sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nakuomba kupitia Bunge lako tukufu, Mheshimiwa Waziti utoe tamko rasmi kwa walimu wetu wote nchini juu ya umuhimu wa wao kufuata Sheria na taratibu za utoaji wa hizi adhabu kwa watoto wetu. Nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya tamko mahususi lililolombwa na Mheshimiwa Mbunge.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa tamko mahususi kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu nafikiri ni muhimu sana na kwanza niseme kwamba utaratibu uliowekwa na sheria wa kuchapa viboko umeainishwa vizuri katika Waraka wa Elimu Namba 24 wa mwaka 2002 uliotengenezwa chini ya kifungu cha 66 cha Sheria ya Elimu. Mwongozo huo pamoja na mambo mengine, umeeleza dhahiri kwamba kuna makosa ambayo ndiyo yataruhusiwa viboko vitumike na siyo kila kosa, kwa hiyo siyo kila kosa mwalimu anaweza akatumia kiboko. Ni makosa makubwa ya kinidhamu na yale yenye sura ya kijinai.

Lakini vilevile kuhusu idadi ya viboko ambayo mwanafunzi anaweza akachapwa, kwa wakati mmoja haitakiwi izidi viboko vinne, lakini vilevile anayeruhusiwa kuchapa ni Mkuu wa Shule au Makamu wake au mwingine yeyote ambae amepewa ruhusa hiyo kwa maandishi.

Lakini kitu kingine cha nne ni kwamba kuchapa viboko ni lazima iombwe na kutolewa kwa maandishi, lakini waraka ule vilevile unasema waziwazi kwamba ni marufuku mwalimu yeyote kutembea na kiboko kwa ajili ya kuchapa wanafunzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, naomba nitoe tamko kwamba ni marufuku mwalimu yeyote kumchapa mwanafunzi kinyume na utaratibu ulioko na sheria, lakini vilevile ni marufuku mwalimu yeyote kuonekana

akitembea na kiboko kwa lengo la kumchapa mwanafunzi na kufanya hivyo ni kuvunja sheria na hatua zitachukuliwa.

Lakini vilevile naomba nitumie nafasi hii kuwaagiza Maafisa Elimu wote wahakikishe kwamba wanagawa Waraka Namba 24 wa Elimu wa mwaka 2002 kwa walimu wote ili waweze kujua taratibu ambazo ainatakiwa zifuatwe kama wanataka kuwachapa wanafunzi. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu, lakini kwenye hili swali la mwisho Mheshimiwa Naibu Waziri mmesema mmewasimamisha kazi hawa watu na kwa sheria zilivyo ni kwamba mtu akisimamishwa kazi hulipwa sehemu ya mshahara pamoja na kwamba anakuwa hajahukumiwa pengine ni vizuri kuangalia utaratibu vizuri ili akiwa kule Serikali isiwe inaingia hasara kwa mtu ambaye ameua mtoto. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nitaleta matangazo tuliyonayo mezani siku ya leo. Kwanza ni wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika; tutaanza na wageni watatu wa Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Job Yustino Ndugai ambao ni Maaskofu wa hapa Jijini Dodoma watakaofanya ibada na Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya maombi ya kufunga mwaka 2018 na hawa ni Mchungaji Gonda, tunaye pia Askofu Amon Kinyunyu, tunaye pia Askofu Yohana Masinga. Karibuni sana viongozi wetu wa dini na tunaamini ibada hii itatusaidia katika mwaka unaokuja pia. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge na kundi la kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Adeladus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambae ni mdogo wake kutoka VETA, Mkoani Mwanza na huyu ni Mwalimu Martin Shigongo Lubangu, karibu sana, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 55 wa Mheshimiwa Zainab Mwamwindi ambao ni kwaya ya Ruaha, Kanisa la Anglikana kutoka Ruaha, Mkoa wa Iringa wakiongozwa na Ndugu Johnson Mgimba. Karibuni sana wanakwaya, mmependeza

sana sijui kama mtatuambia kidogo hapo nje! Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 43 wa Mheshimiwa Lolesia Bukwimba ambao ni wana kwaya wa Kanisa la Anglikana Uvuke, Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wao Ndugu Nicolaus Ndaro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 44 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Said Suleiman Said. Karibuni sana wanamaombi naamini wataungana na Maaskofu wetu kutuombea humu ndani, lakini na Taifa zima kwa ujumla. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambao ni wapigakura wake kutoa Jimboni kwake Kilolo, Mkoani Iringa na hawa ni Ndugu Peter Kisambwe na Ndugu Juma Kandenyela. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni watoto na wake wa Marehemu Chifu Makongoro kutoka Bunda, Mkoani Mara wakiongozwa na mtoto wa Chifu Haruna Makongoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaka kwanza na mama hapo, maelezo ya Mheshimiwa Getere kuhusu wageni hawa anasema chifu huyu, Chifu Makongoro alifariki mwaka 1958 na aliacha wajane 47 na watoto 80 kwa hiyo hawa wageni ni sehemu ya hiyo familia ya marehemu, kwa hiyo Chifu wetu alifanyakazi nzuri kwanza ya kujaza dunia, lakini ya kututengenezea nguvukazi. Ahsante sana Mama na Mheshimiwa Getere anasema yule Mama pale mnamuona pale ama kwa wengine humu ndani ni bibi ana miaka 100. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Afya alivyokuwa anasisitiza hapa kuhusu mazoezi jamani mmemuona mama pale? Hana wasiwasi hata kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Sawa, tuna pia wageni wawili wa Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq ambao ni Makatibu wa Umoja wa Wanawake

- Tanzania kutoka Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma, Ndugu Diana Madukwa na Ndugu Victoria Komba. Karibuni sana viongozi wetu kutoka Chamwino. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanne wa Mheshimiwa Maulid Mtulia ambao ni wadau wa maendeleo ya Jimbo la Kinondoni kutoka *Beleric's Limited* Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mkurugenzi wa Mahusiano Ndugu Aziz Rashid Chonya. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni rafiki zake kutoka Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam na huyu ni Ndugu Warda Obathani ambaye ni Mkurugenzi wa *Arabic Chocolate Cake*. Karibu sana. Na huyu ameambatana na Ndugu Nasra Shaban ambaye ni ndugu yake. (*Makofi*)

Lakini pia tuna wageni wanne wa Mheshimiwa Abbas Ali Mwinyi ambao ni Makatibu wa Matawi ya CCM kutoka Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi wakiongozwa na Katibu Tawi la Michenzani, Ndugu Ibrahim Mwinyi. Karibuni sana viongozi wetu. (*Makofi*)

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, nao ni watumishi watatu kutoka Divisheni ya Taarifa Rasmi (*Hansard*) ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar ambao wamekuja kubadilishana uzoefu na watumishi wa Bunge na hawa ni Ndugu Fatma Msabaha ambaye ni Mkuu wa Divisheni, sijui wamekaa upande gani hawa! Karibu sana. Tunaye pia Ndugu Mohamed Gharib ambaye ni Mhariri wa Taarifa Rasmi, karibu sana. Tunaye pia Ndugu Mariam Juma ambaye ni Mwandishi wa Taarifa Rasmi. Karibuni sana katika kubadilishana uzoefu na wenzetu wa *Hansard* wa hapa Bunge. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 17 ambao ni wanafunzi 14 na walimu watatu kutoka Chuo cha *Evangelistic Central Bible College* cha Ilazo Jijini Dodoma ambao wamekuja kujifunza namna Bunge linavyoendesha shughuli zake. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni kutoka *SHIKANA Law Group* ya Jijini Dar es salaam ambae ni Mkuu wa Shirika hilo ndugu Amne Sued Kagasheki, amekuja kwa ajili ya mafunzo ya kikazi Bungeni. Sijui amekaa upande gani huyu!! Karibu sana sijui kama ni ndugu na Balozi Kagaesheki lakini mpe salama zetu, tunamsalimia sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninayo pia matangazo mengine. Tangazo la kwanza linatoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa *Tanzania Educational Publishers Limited* wanafanya maonesho ya vitabu mbalimbali katika maeneo ya Bunge. Maonesho hayo yanafanyika kati ya Jengo la Utawala na Jengo la Habari. Mnaombwa kutembelea maeneo hayo na kujipatia vitabu na kuona ni vitu gani wanaonesha hapo.

Tangazo lingine Waheshimiwa Wabunge linatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe ambae ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa William Ngeleja wanawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa siku ya Jumamosi tarehe 10 Novemba, 2018 yalifanyika mashindano ya riadha ndefu, lakini kilometa tano katika hiyo *Dodoma Marathon*, Waheshimiwa Wabunge mbalimbali walishiriki lakini Wabunge wetu ambao walikuwa ni vinara ni kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa wanaume aliongoza Mheshimiwa Venance Mwamoto, alifuatiwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka na Mheshimiwa Desderius Mipata alikuwa ni wa tatu. *(Makofi)*

Kwa upande wa wanawake aliongoza Mheshimiwa Kunti Majala, alifuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na wa tatu alikuwa ni Mheshimiwa Susan Kiwanga. Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mbunge wa Mlimba kwenye neema ya chakula. *(Makofi)*

Bunge Sports Club pamoja na Mheshimiwa Waziri wanawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwanza kwa kushiriki, lakini pia kwa kuonesha ushindani ambao ulikuwa ni

mkali sana hawa ndiyo wametuongozea. Ahsanteni sana.
(*Makofi*)

Tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaye ni Mwenyekiti wa ibada, *chapel* ya Dodoma. Anawatangazi Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo kutakuwa na ibada katika eneo la wazi la *basement* mara baada ya kusitisha Bunge sasa hapa ameandika saa 7:00 mchana, naamini ni baada ya kusitisha Bunge sasa.

Aidha, katika ibada hiyo tutakuwa na watumishi wa Mungu, Askofu Kinyunyuu kutoka Kanisa la *Lutheran*, Dayosisi ya Dodoma na viongozi wetu wote tuliowataja walioko Jukwaa la Spika pia watakuwepo. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kwenye hiyo ibada.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 5:26 Asubuhi Bunge Lilihirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 14 Novemba, 2018 Saa Tatu Asubuhi*)